Nipashe
Jumatatu Machi 25, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579874
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Fatma Karume: Nilikwazika kutelekezwa Siku ya Sheria

UKURASA 4




UKURASA 13

# Tanzania yatetema kibabe Afcon 2019

**YAIFUMUA** 3-0 Uganda iliyokuwa haijapoteza hata mechi moja na kuweka rekodi mpya baada ya miaka 39...*Endelea ukurasa wa 32*



Erasto Nyoni (4), akishangilia na wachezaji wenzake baada ya kuzamisha mkwaju wa penalti kimyani kwenye mechi ya kuwania kufuzu Afcon 2019 dhidi ya Uganda kwenye Uwanja wa Taifa jana, hivyo kufuzu michuano hiyo kwa mara ya kwanza tangu 1980. **PICHA: BIN ZUBEIRY**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**SERIKALI KUPOKA HOTELI ZA KITALII**

SERIKALI imeanza ukaguzi wa hoteli za kitalii ilizozibinafsisha kwa wawekezaji na...

UKURASA WA 9

**MENEJA TANROADS KORTINI TUHUMA KUPOKEA RUSHWA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Chato mkoani Geita, imemfikisha mahakamani Meneja...

## Nyama mbovu tani 8 yanaswa

UKURASA 2

# Magereza yakiri tatizo wafungwa kuingiliana

UKURASA 2

**HABARI** FOLENI YA UBUNGO MWISHO NOVEMBA UK. 5

MAONI, KATUNI UK.6

# Tani 8 za nyama ya 'kitimoto' zateketezwa

**Na Mwandishi Maalum,** ARUSHA

SERIKALI imeteketeza shehena ya nyama mbovu za ng'ombe na nguruwe zenye viambata vya sumu zisizofaa kwa matumizi ya binadamu na zilizokwisha muda wa matumizi tani nane zilizoingizwa nchini kwa njia za panya na kuhatarisha afya za wananchi.

Pia nyama hizo zimekamatwa zikiuzwa katika maduka makubwa (Supermarkets) mbalimbali, licha ya kutofaa kwa matumizi ya binadamu pia zimeingia nchini bila vibali, kulipiwa ushuru wa serikali na wala kuhakikiwa ubora wake, huku nyingine zikiwa hazina nembo wala taarifa yoyote katika vifungashio.

Akizungumza wakati akishuhudia uteketezaji wa nyama hizo Njiro jijini Arusha, juzi, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema kukamatwa kwa bidhaa hizo ni sehemu ya matokeo ya operesheni Nzagamba iliyowezesha kukamatwa na kuteketezwa kilo 26,295 za nyama mbovu na maziwa zilizokuwa zimeingia nchini kinyume cha sheria.

Waziri Mpina alitoa onyo kali kwa wafanyabiashara kutambua kuwa serikali iko macho wakati wote na imejipanga kudhibiti uhalifu huo na kwamba hawatapata tena nafasi ya kuingiza bidhaa hizo nchini bila kukamatwa kwa kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka vizuizi kila mahali kufuatilia mtandao haramu wa biashara hiyo na kuutokomeza.

"Hakuna muujiza ambao watautumia wa kuendelea na mchezo huu wa kuingiza nchini bidhaa za mifugo ambazo hazijakaguliwa, bila vibali, zilizokwisha muda wa matumizi, zinazokwepa kodi, hatutachoka kuwakamata na kutaifisha mali zao, hatutachoka kuwapiga faini na kuwapeleka mahakamani, hatutachoka kuendelea kuteketeza mitaji yao na kwamba ili kujiepusha na mgogoro na serikali nawasihi sana wafuate sheria," alisema.

Aliwaagiza watendaji wote wa serikali kuwa makini maeneo yote ya mipaka ili kuhakikisha biashara inayofanyika ni ile ya haki kwa kuwa serikali haijakataza wafanyabiashara kuagiza mazao ya mifugo kutoka nchi za nje.

Waziri Mpina pia aliwaonya wafanyabiashara ambao ni wakiukaji wa sheria wasiingize uhalifu wao kuleta taharuki kwenye uhusiano wa nchi za Afrika Mashariki kwa kuwa ushirikiano uko wa kutosha.

"Watu hawa wachache wasitake kutumia uhalifu wao kwa ajili ya kuchonganisha uhusiano mzuri uliojengeka kwa muda mrefu baina ya mataifa haya kwa kisingizio cha kuhusisha uhalifu wao na uhusiano wetu na kwamba wahalifu wataendelea kubeba msalaba yao wenyewe," alisema.

Alisema Mtanzania yeyote atakayekwenda nchi za nje na kuvunja sheria za nchi hizo atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zilizowekwa kwenye mataifa hayo, vile vile wageni kutoka mataifa hayo wakiingia nchini na kuvunja sheria watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Msimamizi wa Operesheni Nzagamba, Dk. Sophia Mlote, alizitaja baadhi ya mbinu zinazotumika kufanikisha uhalifu huo kuwa ni pamoja na bidhaa nyingi za mazao ya mifugo kuingia nchini kupitia njia za panya kwa lengo la kukwepa ukaguzi, ushuru na zuio la serikali.

Nyingine ni uingiza nchini bidhaa za mifugo zinazokaribia kwisha muda wa matumizi ambazo hununuliwa kwa bei ya kutupa huko nje ya nchi na kwa kukosa soko sehemu nyingine duniani na kisha kuingizwa nchini na baadaye kuuzwa zikiwa zimekwisha muda wa matumizi.

Kwa upande wake Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichalwe, alimhakikishia Waziri Mpina kuwa wataendelea kusimamia kikamilifu majukumu yao kwa mujibu wa sheria ili kuhakikisha udanganyifu na njama kama hizo hazitokei tena nchini.

"Sisi kama watendaji wa serikali tuliopewa dhamana ya kusimamia sekta hii tunakuhakikishia kuwa tutakuwa macho wakati wote kuwasaka wahalifu hawa na kwamba hawataweza tena kuendelea kuwaumiza Wa-

INAENDELEA UK. 8




Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, akisisitiza jambo kwa wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Sekta ya Ujenzi (hawapo pichani), wakati akihutubia baraza hilo mjini Dodoma. **MPIGAPICHA WETU**

## Wafungwa wa kiume wadaiwa kuingiliana kimwili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAFUNGWA wa kiume katika Gereza la Mkoa wa Shinyanga (Mhumbu), wamedaiwa kufanya ngono kinyume na maumbile, hali inayoelezwa kuchangia maambukizi ya magonjwa ikiwamo virusi vya Ukimwi.

Ofisa wa Dawati la Jinsia la Magereza mkoani Shinyanga, Victoria Kizito, alitoa madai hayo kwenye mkutano wa wadau wa kupinga masuala ya ukatili wa kijinsia, ulioandaliwa na Shirika la Agape, Cuso na TGNP.

Alisema elimu hiyo ya ukatili wa kijinsia inapaswa pia kutolewa kwa wafungwa gerezani, ambao wamekuwa wakiingiliana kimwili kufanya ngono kinyume na maumbile hasa kwa wale ambao wameshtakiwa kwa makosa ya ubakaji.

"Naomba elimu hii ya masuala ya ukatili wa kijinsia, pia iwe inatolewa kwenye magereza ambako kuna wafungwa wa kiume wamekuwa wakifanyana ngono kinyume na maumbile, hasa wale waliofungwa kwa makosa ya ubakaji," Kizito alisema.

Mtoa mada kwenye mkutano huo, Rehema Makeba, kutoka TGNP Mtandao, aliwataka maofisa Ustawi wa Jamii mkoani humo wapange mipango kazi yao ya kuwa wanatembelea maeneo mbalimbali na kutoa elimu hiyo ya ukatili wa kijinsia, ikiwamo shuleni na kwenye magereza.

Nao maofisa Ustawi wa Jamii mkoani humo akiwamo Elizabeth Mweyo wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini na Liliani Kiyenze wa Manispaa ya Shinyanga, walikubaliana na wazo hilo na kuahidi kuanza kutoa elimu hiyo ya ukatili na kutoka ofisini.

Aidha, walisema tatizo linalowakwamisha kwenda kutoa elimu hiyo ni ufinyu wa bajeti kutokana na serikali kutotoa kipaumbele cha fedha kwenye idara hiyo ya Ustawi

INAENDELEA UK. 8


JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
22/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwasiku ya Jumanne tarehe26-03-2019 kampuni ya Intercity Builders Limited itasafirisha Mashine kubwa Kutoka Iringa kwenda Bagamoyo gari hilo lenye namba za usajili:
   **T390 BDC NA Tela T984 DAH**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 17 |
| Upana | - | mita | 2.8 |
| Kimo | - | mita | 4.5 |

3. Njia takayotumika **Iringa - Dodoma - Morogoro - Chalinze - Msata - Bagamoyo.** Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115134102


# Mradi wa NSSF, PPF wawaliza wakulima

**Na Salome Kitomari**

WAKULIMA wa miwa katika Kijiji cha Mbigiri, Dakawa wilayani Kilosa mkoani Morogoro, wameiomba serikali kuwasaidia kupata soko la miwa waliyolima kwa lengo la kuuza kwenye Kiwanda cha Sukari cha Mbigiri kilichosimamisha ujenzi.

Kiwanda hicho kilianza kujengwa mwaka 2016 na Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa kushirikiana na uliokuwa Mfuko wa PPF, chini ya Kampuni ya Mkulazi, wakiwa na lengo la kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka.

Wakulima hao waliwaambia waandishi wa habari kwa nyakati tofauti kuwa waliitikia wito wa viongozi mbalimbali wa serikali waliotembelea kiwanda hicho mwaka 2017, wakalima miwa ili kukiuzia kiwanda lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea.

"Tulihamasishwa kulima miwa kabla ya ujenzi wa kiwanda kuanza na sasa tumepoteza nguvu na rasilimali zetu na bado tunadaiwa Sh. bilioni mbili na Benki ya Azania iliyotupa mtaji wa kufanya kazi hii, ni hasara sana kwetu," mmoja wa wakulima hao alisema.

Walisema kwa sasa ujenzi wa kiwanda hicho unasuasua na hakuna anayejua kitakachoendelea na walichukua mikopo ili kuzalisha miwa kwa wingi.

"Kampuni ya Mkulazi Holdings na viongozi wa mifuko na serikali walituhamasisha tulime miwa, tulilima na tulichimba visima hadi leo hatuwaoni wakija, miwa inakauka, visima vina maji hawajayapima, sasa tumebaki kama yatima na hatujui nini cha kufanya," John Mwenda, mkulima wa miwa alisema.

Alisema Mkulazi ambao waliwahamasisha kulima wamenyamaza na hata benki iliyowakopesha haiwapi jibu la wapi watapeleka miwa hiyo, lakini bado wanawadai fedha walizowakopesha.

Mkulima Omari Juma alisema mazao yao sasa yanafikisha miaka miwili yako shambani bila kuwa na mnunuzi na hakuna dalili za kiwanda hicho kuanza kazi siku za karibuni.

Naye Mariam Athuman alisema amefanya kibarua kwa muda mrefu bila kulipwa fedha zake kwenye mashamba ya miwa na hajui lini atalipwa kwa kuwa wamiliki wa mashamba wanasubiri soko.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mkulazi Holdings, Dk. Heldaritha Msita, alisema serikali iko katika mpango wa kununua mitambo ya kiwanda hicho.

Alisema kwa sasa kuna tatizo kwa kuwa wakulima walishalima miwa na imeshakuwa tayari kwa ajili ya kuvunwa.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kebwe Steven, aliwataka wakulima hao kuwa na subira kwa kuwa serikali iko kwenye hatua ya ununuzi wa mitambo ya kiwanda, akiahidi kiwanda kitakuwa kinafanya kazi ndani ya mwaka huu.

Mwaka 2016, NSSF ilieleza kuwa imeelekeza nguvu kwenye viwanda ikiwa ni viwanda vya sukari vya Mkulazi, Ngererege na Mbigiri, Dakawa mkoani Morogoro ambavyo vitazalisha tani 250,000 za sukari kwa mwaka na kutoa ajira kwa zaidi ya watu 100,000.

NSSF pia iliwekeza fedha kwenye viwanda vya nafaka mchanganyiko vya Dodoma na Mwanza kwa kushirikiana na Bodi ya Mazao Mchanganyiko, lengo likiwa ni kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano kwenye viwanda ili kuongeza ajira na kufikia malengo ya nchi ya viwanda.

## HABARI KITAIFA

# Chato kunufaika mradi wa maji wa bilioni 70/-

**Na Renatus Masuguliko,** CHATO

SERIKALI kwa kushirikiana na Serikali ya India itatumia Sh. bilioni 70 kutekeleza mradi mkubwa wa maji katika Wilaya ya Chato, mkoani Geita, utakaowanufaisha wakazi zaidi ya 200,000 ikiwamo shule ya msingi binafsi ya Glory to God iliyopo katika kijiji cha Mulanda, Kata ya Buseresere.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Christian Manunga, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye hafla ya kutoa zawadi na kuwapongeza wanafunzi walioshika nafasi ya kwanza na ya tatu kitaifa katika mtihani wa darasa la nne mwaka jana, kutoka shule binafsi inayofundisha mchepuo wa lugha ya Kiingereza ya Glory to God.

Manunga alisema kuwa baadhi ya kata zitakazonufaika na mradi huo ni pamoja na Buziku, Bwongela na Katende.

Aliitaja kata nyingine kuwa ni Nyalutembo na mradi huo unatarajiwa kuanza baada ya hatua za awali zitakapaokuwa zimetekelezwa, na mwaka 2022 unatarajiwa kuanza kuwanufaisha walengwa.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Vicent Bushaija, aliyekuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, alisema mazingira ya ufaulu wa wanafunzi hao umechangiwa na uwapo wa miundombinu bora na inayokidhi shule ambayo ni majengo, walimu, maji na umeme.

Aidha, Mkurugenzi wa shule hiyo, Diwani Godfrey Mitti, alitangaza neema kwa wanafunzi walioshinda pamoja na kushukuru ujio wa mradi wa maji na umeme kuwa utasaidia kuondoa changamoto zilizopo kwa uongozi wa shule hiyo kumlipia mwanafunzi Bahati Mashine, shilingi milioni moja ikiwa ni ada ya mwaka mzima, huku Elias Musa naye akilipiwa Sh. 500,000 kwa ada ya nusu mwaka,

Wazazi wao wakiwamo Mashaka Fabian na Ernestia Gregoria, waliiomba serikali kutazama namna ya kuzisaidia shule binafsi zinazotoa nafasi bure kwa watoto wenye mahitaji maalum na yatima ili kuwaongezea uwezo wa uendeshaji.

Wanafunzi Bahati aliyeshika nafasi ya kwanza kitaifa na Elias aliyeshika nafasi ya tatu kitaifa katika mtihani wa darasa la nne mwaka jana, kutoka kundi la wanafunzi wasiozidi 40 darasani wote wakitokea shule binafsi ya Glory to God, walisema siri ya mafanikio yao ni uadilifu, kuzingatia maelekezo ya walimu na sala katika maisha yao vimechangia ushindi walioupata.

# Lugola ataka mapambano biashara ya binadamu

**Na Felix Mwagara,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ameitaka Sekretarieti ya Kitaifa ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu nchini, iongeze kasi ya kupambana na biashara hiyo ili iweze kudhibitiwa kwa kuwa inaichafua nchi.

Waziri Lugola, ambaye leo anatarajia kufungua mkutano mkubwa wa mafunzo kwa watekelezaji wa sheria ya kuzuia biashara hiyo haramu, mjini Unguja, Zanzibar, alisema wakati akijiandaa kufungua mafunzo hayo, wahusika waweke mikakati thabiti ya kuidhibiti biashara hiyo.

Mafunzo hayo ya siku tano, yatatolewa kwa wadau wanaotekeleza Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Biashara hiyo, maofisa polisi, Uhamiaji, waendesha mashtaka, mahakimu, maofisa ustawi jamii na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGO), yaliyopo Zanzibar.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii, Waziri Lugola, alisema, mkutano huo ni muhimu kwa wadau hao kupata mafunzo ya kukabiliana na mapambano ya biashara hiyo haramu ambayo wizara yake itaendelea kuidhibiti.

"Nimealikwa kufungua mkutano huo, baada ya mafunzo hayo ya kitaalamu ambayo nimeambiwa yatakuwa ya siku tano, naamini maofisa watakaopewa mafunzo hayo kutoka wizara yangu na maofisa wengine wa serikali kutoka sehemu mbalimbali nchini, pamoja na NGO za hapa Zanzibar watakuwa wamepikwa na kuiva na hatimaye watatusaidia katika kutekeleza sheria ya kuzuia biashara hii haramu ya usafirishaji wa binadamu," Lugola alisema.

Katibu wa Sekretarieti ya Kitaifa ya Kuzuia na Kupambana na biashara hiyo kutoka wizara hiyo, Separatus Fella, alisema zaidi ya washiriki 80 watapewa mafunzo hayo na ana matarajio makubwa elimu watakayopewa itazaa matunda.

Fella alisema washiriki watapewa mafunzo mbalimbali katika semina hiyo na mada mbalimbali zitawasilishwa zikiwamo, washiriki kujua kutofautisha makosa ya biashara haramu ya usafirishaji binadamu na mengine, na namna ya kupeleleza na kuendesha mashtaka.

"Pia washiriki watajifunza namna ya kuwalinda na kuwasaidia waathirika wa biashara haramu ya usafirishaji binadamu, namna ya kuhoji watuhumiwa na mashahidi kwenye kesi za

INAENDELEA UK. 8



18+ DRINK RESPONSIBLY.

# FATMA KARUME: Nilikwazika kutopewa nafasi Siku ya Sheria

**Na Enock Charles**

FATMA Karume (pichani) ni jina kubwa nchini. Haiba yake, ushiriki katika tasnia ya sheria na kiti anachokikalia akiwa ukingoni; Rais wa Chama cha Sheria Tanganyika (TLS), vyote vikoje?

Ana mengi ya ufafanuzi wa nafasi yake, mustakabali wa sheria nchini na yanayohusiana nayo. Fuatilia sehemu ya kwanza ya mahojiano ya Nipashe na mtaalamu huyo wa sheria yaliyofanyika ofisini kwake jijini Dar es Salaam hivi karibuni:

**SWALI:** Ni jambo gani ambalo huwezi kulisahau ndani ya TLS, tarehe za urais wako ukifika ukingoni?

**FATMA:** Eeh! Kwenye historia ya TLS, mimi ni mwanamke wa pili kuwa Rais. Lakini, wa kwanza wa kuchaguliwa na 'immediately' (mara moja) baada ya mimi kupata urais, Chief Justice (Jaji Mkuu) akasimama, akasema hadharani kwamba yeye hayupo tayari kufanya kazi na wanaharakati.

Kwa hiyo, mimi sitosahau hicho kitu na kilinishtusha, kwa sababu 'statement' (kauli) ya kwanza aliyoitoa Chief Justice si kunipa hongera kwa kushinda na nataka uandike hivyo (anasisitiza), ila kuwa hatafanya kazi na mwanaharakati.

Haijawahi kutokea na hajawahi kusema hivyo, Tundu Lissu (mtangulizi wake) akiwa Rais, umesikia? 'So women are judged harder than men' (wanawake wanatathminiwa katika mazingira magumu zaidi kuliko wanaume).

Hakujawahi kutokea 'statement' kama hiyo dhidi ya Rais wa TLS kutoka kwa Jaji Mkuu, ila kwangu kwa sababu ni mwanamke, tena mwanamke niliyekuwa tayari kusema yale yaliyokuwa ya haki na baada ya hapo hajamaliza hapo... 'haja-stop' hapo... hivyo!

Namaliza muda wangu, kahakikisha kwamba sauti yangu... umenisikia? (anasisitiza) kwamba sauti yangu haitapata nafasi yoyote ya kusikika.

Walianiandikia barua kuwa hakuna muda wa mimi kuzungumza na tukumbuke kwamba 'Law Day' (Siku ya Sheria), maana yake ni Siku ya Sheria, umenisikia? Siyo saa ya sheria.

Haijawahi kutokea kwenye historia ya nchi hii kwamba Rais wa Tanganyika Law Society hajapewa muda wa kuongea, ila mimi kwangu imetokea.

**SWALI:** Ni mambo gani makubwa uliyoyafanya TLS na unayaacha kama alama ya uongozi wako?

**FATMA:** Nilipoanza uongozi TLS, nilisema kwamba nitarudi kwenye foundations na 'basics' (misingi) za TLS 'ku-advice' (kuishauri) serikali kuhusu sheria, kuwatetea wananchi, kuwatetea wanasheria wenyewe, pia kuhakikisha kuwa nchi inaendeshwa kwa mujibu wa sheria.



Kwa hiyo, mimi nahisi kwamba kwa kadri ya uwezo wangu kama Rais wa TLS, nimeirejesha TLS kwenye hizo 'fundamentals' (misingi). Tumejitahidi sana kuwatetea wananchi husussan kuhusu matumizi mabaya ya madaraka ya 'ma-regional commissioners' (wakuu wa mikoa), 'District Commissioners' (wakuu wa wilaya), tumetetea sana 'rule of law' (utawala wa sheria).

**SWALI:** Kuna suala la mkanganyiko wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ambayo imelalamikiwa sana na wanasheria mbalimbali wa TLS, mmechukua hatua gani kuhusu hili?

**FATMA:** Hiyo Rebeca Gyumi ameshaipeleka mahakamani. Rebeca ni mwanasheria, ingawa hajawa 'sponsored' (hajadhaminiwa) na TLS. Analishughulikia hilo na kesi hiyo ilianza kabla hata ya urais wangu.

**SWALI:** Tukio la kushambuliwa kwa Tundu Lissu, mtangulizi wako wa TLS, unalielezaje?

**FATMA:** Kwangu mimi binafsi tukio la kupigwa risasi Lissu limenionyesha ubovu wa mfumo, kwamba mbunge ambaye yupo kwenye 'opposition' (upinzani) anapigwa kwa SMG (bunduki) Dodoma ili afe, mpaka leo hajakamatwa mtu.

Hajalipiwa gharama za hospitali, mshahara wake umekatwa. Kwa hiyo, imenifundisha jinsi mfumo wetu ulivyo, kwamba 'chief' (mkuu) wa 'opposition' anashambuliwa siyo kwa kisu, ila kwa 'SMG' mchana katika 'compound' (mazingira) ya serikali, mpaka leo hajapatikana mtu hata mmoja na wala halizungumzwi hadharani.

**SWALI:** Kuna suala la watu waliofungwa maisha. Tumesikia baadhi ya wanasheria kujitokeza kuwatetea. Kama TLS, mna mkakati wowote kuhusu hilo?

**FATMA:** Kwanza, kama TLS, hatuamini kwamba mtu akiua na yeye auawe au kunyongwa. Lakini, mimi binafsi siamini katika kifungo cha maisha kwa sababu 'point' (hoja) ya kumfunga mtu ni ili kumrekebisha, aweze kurudi kuingia kwenye 'society' (jamii) awe 'contributor' (mchangiaji) mzuri, siyo kumfunga ili kumpoteza.

Kwa hiyo, nadhani tatizo lipo kwenye 'interpretation' (tafsiri) pia, kwa sababu siyo lazima ufungwe maisha. Mwingine anachukulia kuwa hana 'discretion' (haki) ya kushuka chini, kwamba lazima ufungwe maisha kwa sababu kufungwa maisha hiyo ni 'maximum' (kiwango cha juu).

Tatizo lipo pia kwenye 'legal aid' (msaada wa kisheria) kwa kuwa serikali ina wajibu kwenye mashtaka ambayo mtu 'either' (ama) ahukumiwe kifo au maisha au zaidi ya miaka fulani.

Kwangu mimi ningekata kwenye miaka mitano kwa sababu nayo ni mingi. Kwa hiyo, lazima serikali ifanye jitihada za kumpatia mwananchi wa kawaida mwanasheria.

Kwa hivi sasa, wanafanya hivyo, lakini 'only' (isipokuwa tu) kwenye kesi zenye hukumu za kifo. utapatiwa mwanasheria na mwanasheria huyo analipwa laki moja kwa kazi yote kwa kesi nzima.

Kwa hiyo, malipo pia ni kidogo sana, lakini kuna baadhi ya wanasheria wema wanajitolea, wanafanya na saa nyingine hata hatulipwi hizo hela.

Mtu anaweza kutoka hapa akaenda Morogoro 'system' (mfumo) yenyewe ni mbaya sana, kwa sababu hatupewi hata 'allowance' (posho) ya kujaribu kutafuta mashahidi, umenielewa eeh (anasitiza)?

Kwa hivyo, ni 'very difficult' (ngumu sana), lakini ni muhimu tuanze kuipa thamani maisha ya watu na tujue kwamba kumfunga mtu hata kuanzia miaka mitatu na juu yake ni kitu kikubwa mno.

Kwa hiyo, mtu huyo kabla hukumu haijafikiwa, ni lazima apewe uwezo wa kujitetea na uwezo wa kujitetea ni kupitia mwanasheria. Unaweza kuniuliza kwa nini TLS hawafanyi hivyo?

Kwa sababu wanasheria wana haki ya kupata malipo kwa kazi wanazozifanya. Kwa sababu kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 22 inasema "kila mtu anayo haki ya kufanya kazi; Ibara ya 23 inasema, kila mtu bila kuwapo ubaguzi wa aina yoyote, ana haki ya kupata ujira unaolingana na kazi yake na watu wote wanaofanya kazi kwa uwezo wao, watapata malipo kutokana na kiasi na kazi walizofanya." Kwa hiyo, sisi kama chama, hatuna uwezo wa kuwalipa wanasheria kuwasimamia wananchi wote kwa sababu TLS inaendeshwa kwa pesa za wanachama wenyewe.

Kila mwanachama anatoa pesa kila mwaka ili chama kiendeshwe. Kwa hiyo hatupati pesa pengine popote, isipokuwa kwa wanachama. Kwa hiyo tuseme, tukiwa tuna 'project' (mradi) fulani kuzifanya, pengine kuna wadau wanaweza kulipia zile 'projects'(miradi). Kinachofanyika, unakuta kunakuwapo wanachama walioguswa na jambo na kuamua kujitolea.

Ninachoweza kusema kuwa ni muhimu kwa serikali kuwa na kitengo cha kuweza kuhudumia wananchi, kwa maana ya kutoa 'legal aid' (msaada wa kisheria) kwenye 'concept' (dhana) ya sheria, kuna kitu kinaitwa 'Access to Justice' (Kiingilio cha kwenye haki ya kisheria). 'So' (hivyo) ni 'duty' (wajibu) ya serikali kuhakikisha watu wanaopata vifungo vya muda mrefu wanaipata hiyo. Lakini, pia sio 'ku-force' (kulazimisha) wanasheria kutoa huduma bure, kwa sababu hiyo ni kinyume cha Katiba.

Sisi tuna 'Legal Aid Act' (Sheria ya Msaada wa Kisheria). Lakini, tunaitizama kama ni watu wa kujitolea kutoa msaada wa bure. Huwezi 'kum- force' mtu kujitolea.

Mfano, Kenya wanatazama uwezo wa mtu kwenye kesi yoyote, halafu 'una-apply' (unaomba) kupata msaada wa kisheria. Wana bodi na serikali kwenye bajeti inaweka bajeti ya 'legal aid.' Kwa, hiyo, Bunge linapasisha halafu inaingia kwenye 'Legal Aid Fund' (Fungu la Msaada wa Kisheria).

Kwa hiyo, kama wewe huna uwezo, unakwenda unaomba usaidiwe kwenye hii 'Legal Aid fund' unapeleka maombi kwa maandishi, halafu wanaitazama kesi yako, wakiona kwamba wewe unastahili kupata 'legal aid' then (hivyo) wanakupa 'lawyer' (mwanasheria) halafu huyo 'lawyer' analipwa. Sio kwamba 'lawyer' anajitolea.

Sisi hapa wengi wanajitolea, isipokuwa kwa kifungo cha kunyongwa tu ambacho pia hulipwa kidogo sana.

***Usikose sehemu ya pili ya mahojiano haya kesho**




# Serikali kupoka hoteli za kitalii

**Na Mwandishi Maalum**

SERIKALI imeanza ukaguzi wa hoteli za kitalii ilizobinafsisha kwa wawekezaji na wale watakaobainika kuziendesha chini ya kiwango, watanyang'anywa na kupewa wawekezaji wengine walio tayari kuziendesha kwa manufaa na kukuza utalii nchini.

Imesema inachukua hatua hiyo kutokana na kuwapo kwa malalamiko kutoka kwa watalii na wadau mbalimbali wa utalii kuhusu huduma zisizoridhisha zinazotolewa na hoteli hizo.

Akizungumza baada ya kukagua baadhi ya hoteli za kitalii zikiwamo Soronera na Lobo zilizoko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti mkoani Mara, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema lengo la kubinafsishwa kwa hoteli hizo lilikuwa kuboresha huduma.

Alisema Hoteli za Musoma mkoani Mara na Ngorongoro Wildllife iliyoko ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ni miongoni mwa zilizofanyiwa ukaguzi.

Kanyasu alisema mwekezaji asiyeboresha huduma, atanyang'anywa umiliki ili kupewa mwekezaji mwingine mwenye uwezo wa kutoa huduma bora.

Alisema kumekuwa na tuhuma kwa baadhi ya hoteli zilizobinafsishwa kukwepa kodi ya tozo ya huduma pamoja kuwalipa wafanyakazi wazawa mishahara midogo, huku wale wa kigeni wakilipwa mishahara mikubwa kwa kazi zinazofanana.

Kanyasu alisema serikali ilizibinafsisha hoteli hizo ili zilete mapinduzi katika nyanja za ajira, huduma bora kwa watalii, kodi na kuziboresha ili zikidhi soko la watalii.

Akizungumza baada ya kukagua hoteli hizo, Kanyasu alibainisha baadhi ya vitu alivyoviona kuwa ni uchakavu wa miundombinu na udanganyifu wa taarifa za idadi ya watalii wanaofika katika hoteli hizo.

Alisema wizara itapeleka kwa Msajili wa Hazina orodha ya hoteli zitakazobainika kwenda kinyume ili zifutiwe umiliki.

Kanyasu pia aliwataka viongozi wa hoteli hizo kukaa na kuona mbinu watakayoitumia kuongeza idadi ya Watanzania wanaotembelea hifadhi na kupata mapumziko katika hoteli hizo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, Victor Tonesha, alisema changamoto inayoikabili halmashauri hiyo ni kushindwa kubaini kiwango halisi cha fedha zinazotolewa na wawekezaji wa hoteli hizo.

# Tarehe matumizi barabara za juu Ubungo yatajwa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKALA wa Barabara (Tanroads) umesema ifikapo Desemba, mwaka huu, magari yanayotumia Barabara ya Morogoro yataanza kupita juu ya daraja eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam.

Vilevile, umesema magari yanayotumia Barabara ya Sam Nujoma kwenda Barabara ya Mandela jijini, nayo yataanza kupita juu ya daraja katika eneo hilo Julai mwakani.

Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Patrick Mfugale, aliyasema hayo jijini mwishoni mwa wiki wakati wajumbe wa Bodi ya Tanroads walipotembelea miradi ya ujenzi inayosimamiwa na taasisi hiyo.

Wajumbe hao walitembelea mradi wa ujenzi wa Daraja la Nyerere (sasa linaitwa Daraja la Selander, jengo la tatu la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), mradi wa barabara za juu eneo la Ubungo na pamoja na mradi wa ujenzi wa barabara sita kutoka Kimara hadi Kibaha.

"Ifikapo mwishoni mwa mwaka huu, yaani Desemba, magari yatakayokuwa yanatoka Kimara kuelekea mjini, yataanza kupita juu ya daraja na yale yanayotoka Mwenge kuelekea Buguruni, yataanza kupitia juu ya daraja Julai mwakani,"

INAENDELEA UK. 8




215135301

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Beki Simba ijipange Caf TP Mazembe inafungika

**HATIMAYE** wawakilishi pekee wa Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Africa, Simba wamejua wapinzani wao katika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Katika droo iliyochezeshwa Jumatano iliyopita Simba iliyomaliza nafasi ya pili katika Kundi D lililokuwa likiundwa na vinara Al Ahly, AS Vita na JS Saoura, sasa itakutana na TP Mazembe ya DR Congo.

TP Mazembe imeingia hatua hiyo baaada ya kuongoza Kundi C na inakumbukwa kwa ushindi wake wa kishindo wa mabao 8-0 dhidi ya Constantine.

Hata hivyo, Simba inabidi kujipanga vizuri kwani ukiacha Al Ahly ambayo ni mabingwa wa kihistoria katika michuano hii kutokana na kuubeba ubingwa mara saba, TP Mazembe ndiyo inayofuata kwa kutwaa kombe hilo mara nyingi.

Wakiwa wamebeba ubingwa huo mara tano, mwaka 1962, 1968, 2009, 2010 na 2015, hivyo si timu ya kuivaa kizembezembe.

Mbali na rekodi hiyo, lakini pia katika hatua ya makundi imemaliza ikiwa na pointi 11, huku ikipoteza mechi moja tu, tofauti na Simba iliyoangukia pua mechi zote tatu za ugenini.

Hata hivyo, tunaimani kubwa na Simba kuweza kuendelea kuipeperusha vema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Lakini wasiwasi wetu ni kutokana na safu yao ya ulinzi kuruhusu mabao mengi ugenini jambo ambalo linaweza kuwagharimu na kujikuta wakiishia hatua hiyo ya robo fainali.

Tunalazimika kuyaeleza hayo mapema kutokana na ukweli kwamba, katika hatua hii ya robo fainali kinachoangaliwa ni tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa baada ya mechi mbili ya nyumbani na ugenini na si pointi tena.

Hivyo, kama Simba haitaweza kujizatiti vema hususan kwenye safu yake ya ulinzi ambayo tulishuhudia ikiruhusu jumla ya mabao 10-0 katika mechi mbili mfululizo za ugenini dhidi ya AS Vita na Al Ahly kila moja ikipigwa 5-0, hakika hapa ndipo panaweza kuwa mwisho wa safari yao kwenye michuano hiyo.

Ingawa pia kama itajipanga vema inaweza kufuta makosa hayo na kufika nusu fainali kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1974.

Tunaamini hilo linawezekana kwa maandalizi kuanzia sasa kabla ya mechi ya mkondo wa kwanza Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Matumaini yetu hayo yanaongezeka kutokana na ukweli kwamba kwa sasa kiwango cha TP Mazembe hakitofautiani sana na mahasimu wao, AS Vita ya DR Congo waliokuwa kundi moja na Simba.

Hiyo ni kutokana na kwenye Ligi Kuu ya DR Congo mapema mwezi huu, Machi 3, AS Vita iliiangushia kipigo cha mabao 3-0, mechi hiyo ikiwa ni ya marudiano baada ya ile ya mzunguko wa kwanza TP Mazembe kushinda 3-2 Novemba 4, mwaka jana.

Kwa rekodi hizo, kama Simba iliweza kuichapa AS Vita hapa nchini kwa mabao 2-1, hilo linawezekana pia kwa TP Mazembe endapo itajipanga vema.

Tunafahamu TP Mazembe itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya rekodi nzuri zilipokutana mwaka 2011 kwenye michuano hiyo na Simba kuangukia pua Uwanja wa Taifa kwa mabao 3-2 kabla ya ugenini kuchapwa 3-1, lakini hilo halitupi hofu kabisa.

Nipashe tunaamini rekodi zipo kwa ajili ya kuvunjwa na Simba huu unaweza kuwa mwaka wao wa kuzivunja kama itajipanga vema na kupata ushindi mkubwa nyumbani kabla ya kwenda kuhitimisha kazi hiyo ugenini. Hivyo tunaitakia maandalizi mema kuelekea mechi hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

**BUSARA**

**WIMBI LA KUNAJISI WATOTO LATOKA WAPI**
**IELEZWE KWA NAMNA YOYOTE NA KWA LUGHA YOYOTE ILE, KUWANAJISI WATOTO NA VIKONGWE NI UNYAMA JUU YA UNYAMA. NI UDHALILISHAJI USIO NA KIFANI. KAMA NI SHETANI ALEGEE, KAMA NI USHIRIKINA UTOKOMEE. KWA JINA LA TANZANIA!**
**NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kamati ya kuhamasisha isiishie Taifa Stars tu

**KABLA** ya mechi ya Taifa Stars dhidi ya Uganda iliundwa Kamati ya Ushindi ili kuhamasisha Watanzania kwenye mechi hiyo muhimu iliyochezwa jana.

Iliitwa "Kamati Saidia ya Taifa Stars Ishinde", ambayo iliundwa na wanasiasa, wafanyabiashara, viongozi, wanamichezo na watu wa kada mbalimbali.

Kwenye hamasa, kamati hii ilijitahidi kupita maelezo. Ilileta hamasa haswa na hata wale waliokuwa hawajui nini kinaendelea, walijua kuwa kuna mechi kati ya Stars dhidi ya Uganda kufuzu Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 nchini Misri.

Napenda kuwapongeza wote waliokuwa kwenye kamati hii kwani walifanya kazi yao ipasavyo, kuwaunganisha Watanzania kuwa kitu kimoja, kusahau tofauti zao za kiitikadi za klabu zao na hata vyama na kuongea lugha moja tu ya kimichezo.

Pamoja na hayo, binafsi naona kitendo hicho kilichelewa sana na badala yake kingeanza kabla hata ya mechi ya kwanza kabisa dhidi ya Lesotho.

Ikumbukwe mechi ya kwanza ya Afcon ilichezwa Juni 10, 2017, kwenye Uwanja wa Azam Complex na Stars ikalazimishwa sare ya bao 1-1.

Nakumbuka mechi hii ilichukuliwa poa tu, ilionekana kama mechi ya kawaida, Stars ikipelekwa Chamazi na wala hakukuwa na mashabiki wengi kihivyo, wala hamasa kiasi cha kuambulia sare.

Nafikiri kama kuanzia mwanzo kungekuwa na hamasa kama hii, mechi hiyo Stars ingeshinda bila matatizo na kabla hata ya mechi dhidi ya Uganda ingekuwa imeshafuzu zamani.

**Hamasa iliyoonekana kuelekea mechi dhidi ya Uganda igeukie kwa upande wa pili, ielekee kwa vijana wa Serengeti Boys na kinadada wa Twiga Stars ili hata wao waone hakuna upendeleo kwenye kusaka ushindi kwa ajili ya sifa ya nchi.**

Kwa maana hiyo tuna la kujifunza kuwa wakati mwingine mambo kama haya tuyaanze mapema.

Tumeona Simba walivyofanya kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika. Walianza tangu mwanzo kuhakikisha wanashinda mechi zote tatu za nyumbani. Na ndizo zilizowapeleka robo fainali. Wangezinduka kwenye mechi ya mwisho, saa hizi wangekuwa nje. Haya yameshapita, Tanzania tuna michuano mingine ya kimataifa.

Kwanza kuna fainali za Afcon kwa vijana chini ya miaka 17, inayotarajiwa kufanyika nchini kuanzia Aprili 14 hadi 28, mwaka huu.

Timu yetu ya Serengeti Boys itashiriki michuano hiyo kama mwenyeji.

Lakini pia Timu ya Taifa ya Wanawake 'Twiga Stars' kwa sasa ipo kambini kujiandaa kufuzu kwa michuano ya Olimpiki itakayofanyika mwakani nchini China.

Kinadada wa Kibongo Aprili 5, wanatarajia kucheza dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), kabla ya mechi ya marudiano ugenini.

Ushauri wangu ni kwamba kamati hii ilioundwa isiishie kwa Taifa Stars tu, bali iendelee kwa timu zetu za taifa zilizobaki ili nao wajihisi ni sehemu ya taifa na wanathaminiwa.

Hamasa iliyoonekana kuelekea mechi dhidi ya Uganda igeukie kwa upande wa pili, ielekee kwa vijana wa Serengeti Boys na kinadada wa Twiga Stars ili hata wao waone hakuna upendeleo kwenye kusaka ushindi kwa ajili ya sifa ya nchi.

Ni muhimu sasa kuangalia uwezekano wa kamati hizi kuanza kufanya kazi yake mapema wakati wa maandalizi wa michuano yoyote ile, lakini iwe kwa timu zote za Taifa na za jinsi zote pia. Hili ni kwa maslahi mapana ya taifa.

## MJADALA

# Kujikomboa kwa Yanga ni kufanyika uchaguzi

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, Klabu ya Yanga kwa kipindi hiki imekuwa vigumu kufanya uchaguzi tofauti na vipindi vingine huko nyuma.

Shirikisho la Soka nchini (TFF) lilisema, Baraza la Michezo (BMT) likasisitiza, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo likatilia mkazo, lakini baadhi ya wanachama wa klabu hiyo wakakimbilia mahakamani kupinga uchaguzi kufanyika.

Ni haki yao, lakini wanachama hawa hawakuangalia maslahi mapana ya klabu na badala yake wakaweka zaidi maslahi yao binafsi, pamoja na mihemko.

Nadhani Yanga ingefanya uchaguzi haraka kama kitu kimoja tu kingefanyika. Shirikisho la Soka Duniani (Fifa) kama ingeagiza hivyo, kwa sababu hawana masihara wala kujuana. Wakisema vinginevyo tutawafungia miaka mitatu, basi wamemaanisha.

Naweza kusema kitu kimoja tu kuwa Yanga imechelewa hadi leo kufanya uchaguzi kwa sababu za kisiasa zaidi, vinginevyo sasa hivi ingekuwa imeshafanya hivyo.

Sidhani kama ingekuwa klabu nyingine ya kawaida inapiga danadana hivi ingechwa.

Inaonekana kama vile kuna watu wananufaika na ukata uliomo kwenye klabu hiyo kwa sababu badala ya kutafuta mbinu za kuondoa, wao wanachofanya ni kutembeza bakuli kwa wanachama na mashabiki watoe chochote ili kuisaidia timu.

Staili hii ya kuchangishana pesa ambayo Yanga wanaitumia kwa sasa haionekani kabisa kuwa itamaliza matatizo ya ukata uliomo kwenye klabu hiyo.

Kabla hata Yanga haijajiweza kiuchumi, hakuna mwaka wowote ambao ilichangisha wanachama na mashabiki kwa ajili ya kuendesha klabu, bali ilikuwa na viongozi wenye maono ambao walikuwa wakiweka mikakati ya wapi kwa kupata pesa ya kuifanya klabu isonge mbele.

Kwa klabu kubwa kama Yanga hata siku moja pesa za kuchangishana kwa dizaini iliyopo sasa haiwezi kutosha.

Kama ingekuwa klabu kama Ndanda, Stand United, Mbao FC na zingine sawa kwa sababu kwa kawaida hazina matumizi makubwa ya posho na mishahara ya wachezaji kama zilivyo Klabu za Simba, Yanga na Azam.

Ikumbukwe kuwa Yanga imesheheni wachezaji wenye viwango na gharama kubwa, wa ndani na wa nje, wengine wakiwa wanamaliza mikataba yao, sidhani kwa staili hii kama inawezekana kuwasajili tena kwa pesa hizo za kuchangishana.

Kinachotakiwa kwa sasa Yanga ni kufanya uchaguzi ili kuwapata viongozi ambao watakuwa na mikakati ya kuhakikisha klabu inajiendesha yenyewe bila kuomba, lakini pia kuhakikisha wanachama na mashabiki wanaichangia klabu kwa mtindo mwingine kama vile kununua jezi, kalenda, na bidhaa zingine za klabu, kujazana viwanjani wakati timu inacheza, pia kutafuta wadhamini.




Kwa sasa hakuna mdhamini yeyote atayewekeza pesa zake kwenye klabu hiyo kwa sababu hakuna kiongozi wa kuchaguliwa.

Kuchangishana pesa kwa staili hii ilionekana kama mkakati wa muda mfupi tu kuitoa klabu sehemu moja kwenda nyingine, lakini inavyoonekana ni kama baadhi yao wanaona kama iwe ndiyo mfumo wa maisha ya klabu kiasi cha eti kuunda hadi kamati.

Je, kuna baadhi ya watu wananufaika na hizi pesa zinazochangwa viwanjani na wanachama na mashabiki kiasi kwamba baadhi yao wanaona ni bora kusiwapo uchaguzi ili waendelee kunufaika?

Sijui, lakini ili kuionea huruma klabu na kurejea kwenye hali yake ya kawaida ni lazima kwanza uchaguzi ufanyike na wapatikane viongozi wapya watakaokuwa na maono mapana ya kuendeleza klabu hiyo kongwe, lakini si kwa staili hii.


## BONITE BOTTLERS LIMITED

### Advertisements of Employment

**1. Area Sales Supervisor**

**Qualification:**
- Applicant should be a holder of Bachelor of Commerce in Marketing / Business Administration or any other related field from recognized Institution.

**Key Skills & Abilities:**
- Ability to manage and monitor staff performance to ensure the preset targets are met
- Ability to actively pursue opportunities to improve Route to Market and leveraging best practices.
- Ability to drive horizontal expansion through outlet creation incentive programs
- Ability to identify Commercial and Market development improvement initiatives to drive incremental volume, and profit share.
- Ability to track performance against objectives regularly and initiate corrective measures.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated, flexible person and a good team player

- **Experience** : Any experience in related field will be added advantage.
- **Location** : Arusha & Kilimanjaro

**2. Salesman**

**Qualification:**
- Applicant should be a holder of form IV/VI with Diploma in Sales and Marketing / Business Administration or any related field from recognized Institution.

**Key skills & Abilities:**
- Skills and knowledge of customer care and customer services.
- Ability to forecast sales/load to be taken for each day to the location assigned.
- Able to work independently with minimum supervision.
- Self motivated, flexible person and a good team player.
- Ability to seek out and develop new business and maximize all possible opportunities to increase Sales

- **Experience : Any experience in the same field will be added advantage**
- **Location : Arusha & Kilimanjaro**

**Mode of Application:**
All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to undersigned address, reach him not later than 28/03/2019.

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI.**
**E- mail hr@bbl.co.tz**

215135602



## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO

## PATA KIWANJA JIJINI DODOMA

**22/03/2019**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anapenda kuwatangazia Wananchi wote kuwa, Halmashauri kwa kushirikiana na Kampuni ya Khakasa Ltd imekamilisha upimaji wa viwanja vya matumizi mbalimbali katika eneo la Nala, Barabara Kuu ya Dodoma-Singida na vitauzwa kuanzia tarehe 25/03/2019 katika eneo la wazi lililopo kwenye Ofisi za Manispaa ya zamani jirani na Sabasaba.

Mchanganuo wa bei na muda wa malipo ni kama inavyoonekana kwenye jedwali.

| Na. | Matumizi | Bei (kwa mita moja ya mramba) | Muda wa malipo | Eneo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Makazi | 5,000 | Miezi Mitatu | Nala-Lugala |
| 2 | Biashara | 6000 | Miezi Mitatu | Nala-Lugala |
| 3 | Makazi na Biashara | 5,500 | Miezi Mitatu | Nala-Lugala |
| 4 | Taasisi | 6,000 | Miezi Mitatu | Nala-Lugala |

Aidha, kila anayehitaji kiwanja afike katika Ofisi na tarehe tajwa hapo juu ili akamilishe taratibu za kumilikishwa kiwanja Jijini Dodoma, Makao Makuu ya Nchi. Kwa mawasiliano zaidi piga namba 0714785513.

**Tangazo hili limetolewa na:**

**Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

115135802

## Wafungwa wa kiume wadaiwa

INATOKA UK. 2

wa Jamii, ikiwa asilimia kubwa wakiyategemea mashirika kuambatana nao kwenda kutoa elimu hiyo.

Kwa upande wake Ofisa Miradi kutoka Shirika la Agape mkoani Shinyanga, Mustapha Isabuda, ambao wanajishughulisha na kupinga ukatili kwa watoto na wanawake, alisema wameitisha mkutano huo ili wadau wapate kujadili namna ya kupunguza ukatili wa kijinsia mkoani Shinyanga ambao ni asilimia 78 kwa mkoa wa Shinyanga na kitaifa 50.

## Lugola ataka mapambano

INATOKA UK. 3

biashara haramu ya usafirishaji binadamu," alisema Fella.

Aidha, katika ufunguzi wa mafunzo hayo ambayo mgeni rasmi atakuwa Waziri Lugola, Fella alisema pia maofisa mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar watashiriki kwenye hafla ya ufunguzi huo.

Aliongeza kuwa, mafunzo hayo ni kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Marekani linalojihusisha na Masuala ya Utafiti (RTI).



Mtaalamu wa macho kutoka Hospitali ya Macho ya CCBRT, Cyprian Ntomoka, akimpima macho mfanyakazi wa Tigo, Isaack Shoo, kwenye zoezi la upimaji macho na masikio lililofanywa na hospitali hiyo bure kwa wafanyakazi wa Tigo wa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

## Tani 8 za nyama ya 'kitimoto'

INATOKA UK. 2

tanzania, tutaendelea kuwakamata kabla ya kuwafikia walaji na kodi na ushuru wote wa serikali kukusanywa," alisema Sichalwe.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alimshukuru Rais Dk. John Magufuli, kwa uamuzi wa kuunda Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kumkabidhi Waziri Mpina kwa kuwa kwa kipindi kifupi alichoiongoza wizara hiyo mambo mengi ya ajabu yamefichuka.

Pia ameagiza kufuatiliwa kwa maofisa wa serikali waliokuwa mipakani na kujua ni kwa nini waliruhusu bidhaa hizo kuingia nchini kinyume cha sheria ili hatua kali zichukuliwa dhidi ya watendaji hao wa serikali kwa lengo la kutokomeza mtandao huo.

Mwanasheria wa Bodi ya Nyama, Praygod Lukio, alisema kuingiza bidhaa zilizokwisha matumizi na kuuza ni kosa la uhujumu uchumi na adhabu yake ni kifungo cha miaka 14 jela, hivyo ni vyema wafanyabiashara wakatii sheria kwa kuwa kuna wakati serikali haitatumia tena mbadala wa kutoza faini.

# Anayedaiwa kuchoma bendera, katiba ya CUF ashtakiwa

**Na Boniface Gideon,** TANGA

CHAMA cha Wananchi (CUF), Wilaya ya Tanga, kimemburuza mahakamani aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Rashidi Jumbe, kwa kosa la kuchoma moto bendera na katiba za chama hicho muda mfupi baada ya aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho Maalim Seif, kutangaza kujiunga na Chama cha ACT-Wazalendo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Usalama wa CUF Taifa, Masoud Mhina, alisema chama hicho kimeamua kumfungulia kesi mwenyekiti huyo Mahakama Kuu, Kanda ya Tanga, kwa kosa la kuchoma nyaraka ambazo ni mali za chama hicho.

Pia alisema chama kinamdai mali mbalimbali za chama ambazo ameshindwa kuzirudisha wakati alipokuwa anatangaza kuhama chama.

Alisema baadhi ya mali wanazomdai ni pamoja na spika, meza, viti na mali nyingine. "Naomba niwaambie ukweli kwa wote waliohusika kwa namna moja ama nyingine kuharibu mali za chama tunawachukulia hatua kali za kisheria, tunaanza na huyu Rashid

Jumbe, tumeshamfungulia kesi mahakamani na anashikiliwa na Jeshi la Polisi, tunaendelea na uchunguzi mpaka tuwabaini wale wote walioshiriki kukihujumu chama chetu," alisema.

Kwa upande wake mwenyekiti mpya wa chama hicho, Mambea Pashua, alisema wamekubaliana na madiwani wote wa chama hicho waliopo katika Halmashauri ya Jiji la Tanga kuwa hawatakihama chama hicho.

"CUF haimzuii mwanachama wake asikihame chama, kwa kuwa kuhama chama ni haki ya kikatiba, lakini kwa kuwa sisi tuna mapenzi na chama chetu, hatukihami hata kwa dawa, tutaendelea kusimama imara ili kukiimarisha chama chetu kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwakani, sisi CUF hatuburuzwi na mtu," Pashua alisema.

Alisema kitendo kilichofanywa na baadhi ya waliokuwa wanachama wake sio cha kiungwana.

Kwaupande wake Diwani wa Kata ya Mnyanjani (CUF), Thobias Haule, alisema hayuko tayari kukihama chama hicho kwa kigezo cha kumuunga mkono mtu.

Nao baadhi ya wakazi wa Jiji la Tanga, Ally Mohamed na John Masha, walisema licha ya CUF kipitia katika wakati mgumu, bado chama hicho kina nguvu kubwa kwa wananchi.






## Tarehe matumizi barabara za juu

INATOKA UK. 5

Mfugale alisema.

Meneja wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyover) katika makutano ya barabara ya Ubungo, Barakaeli Mmary, alisema kuwa hadi sasa, ujenzi wa barabara za pembeni umekamilika kwa asilimia 70 na upanuzi wa madaraja umekamilika kwa asilimia 80.

Alisema kazi ya kuhamisha miundombinu iliyokuwa imepita katika eneo la mradi kama vile gesi, umeme, maji na simu inaendelea na imeshafanyika kwa asilimia kubwa.

"Tumeshahamisha miundombinu ya maji kilometa 2.6, umeme kilometa 17, gesi kilometa 1.2, simu kilometa 2.6, ambayo ilikuwa ardhini, bado tunaendelea kuhamisha, wataalamu wa miundombinu hiyo wamekuwa wakikutana mara kwa mara," Mmary alisema.

Alisema jumla ya nguzo 130 zimeshachimbiwa na nguzo nne kubwa kati ya 60 zimeshachimbiwa katikati ya makutano ya barabara.

Mmary alisema daraja hilo litakapokamilika, litakuwa na ngazi tatu, na kwamba ngazi ya kwanza ujenzi wake umeshakamilika kwa asilimia 80, ngazi ya pili itakamilika mwishoni mwa mwaka, na ngazi ya tatu itakamilikia Julai mwakani.

Alisema kutengenezwa kwa mzunguko wa magari (Round about) eneo la Ubungo kumepunguza msongamano wa magari kwa kiwango kikubwa.

Machi 20, mwaka jana, Rais John Magufuli aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara hizo katika makutano ya Ubungo utakaochukua miezi 30 na kueleza kuwa mradi huo utagharimu Sh. bilioni 188.71 ukiwa na lengo la kupunguza msongamano wa magari katika Barabara za Morogoro, Nelson Mandera na Sam Nujoma.

Rais Magufuli aliitaka Kampuni ya China Civil Engineering Construction Cooperation (CCECC) iliyopewa zabuni hiyo, kuhakikisha ujenzi unafanyika usiku na mchana ili kukamilisha kwa wakati mradi huo.

# Wananchi waiomba polisi kukomesha biashara ngono

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WANANCHI katika Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuingilia kati suala la biashara haramu ya ngono ambayo imeshamiri katika wilaya hiyo.

Wananchi hao walitoa ambi hilo wakati wakizungumza na gazeti la Nipashe kwa nyakati tofauti kwa sharti la kutotajwa jina gazetini, huku wakieleza kuwa kitendo cha Jeshi la Polisi kutolipatia ufumbuzi suala hilo wakati maeneo yaliyoshamiri kwa biashara hiyo yakifahamika kutasababisha wananchi kutokuwa na imani na jeshi hilo.

Walisema kuwa kutokana na biashara hiyo kufanywa waziwazi, inaweza kuletea kuongezeka kwa maambukizo ya virusi vya Ukimwi katika wilaya hiyo na kusababisha kuporomoka kwa maadili ya watoto.

Walisema kuwa katika Wilaya ya Kahama, biashara hiyo imeshamiri katika Viwanja vya Soko la Wakulima, maarufu kama Lumambo, na katika nyumba ya kulala wageni (jina linahifadhiwa). Wananchi hao walilalamikia Jeshi la Polisi wilayani humo kulifumbia macho suala hilo wakati vitendo hivyo vikifanyika wazi katika maeneo yaliyotajwa ambayo yanatumika kama dangulo. "Serikali inaruhusu biashara ya madanguro? Na kama hairuhusu je, kwanini inashindwa kuchukua hatua kwa mmiliki wa nyumba hiyo ya kulala wageni?" Alihoji mmoja wa wananchi ambaye aliomba jina lake lisitajwe.

Mwananchi mwingine ambaye hakutaka kuandikwa jina gazetini, alisema kuwa kwa kitendo cha serikali kutolichukulia hatua za kisheria suala hilo ni sawa na kuruhusu kuendelea kwa biashara hiyo haramu.

"Mimi kama mwanamke kwa kweli kitendo wanachokifanya wanawake wenzangu cha kuuza miili yao ni kutudhalilisha wenzao na kutusababishia kutuletea magonjwa nyumbani, lakini pia tutakuwa hatuna imani na waume zetu, naomba serikali itunusuru kama ilivyowanusuru wananchi wa Dodoma kwa kuwaondoa kwa nguvu wanaojiuza," alisema. Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akiwahutubia wananchi katika Siku ya Ukimwi Duniani, iliyofanyika katika viwanja vya Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, alikemea vitendo vya wanawake kujiuza, huku akiliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata wanaume wanaofika katika nyumba hizo kwa lengo la kununua madada poa. Macha alisema kuwa iwapo Jeshi la Polisi wilayani humo litafanya hivyo vitendo vya wanawake kuuza miili yao litapungua kwa kasi kubwa kutokana na kuwakamata kinababa poa na dadapoa.

# Meneja Tanroads kortini tuhuma kupokea rushwa

**Na Daniel Limbe,** CHATO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Chato mkoani Geita, imemfikisha mahakamani Meneja Msimamizi wa Mizani ya Magari Bwanga, Daud Kadinilo, akikabiliwa na tuhuma za kufanya makosa ya kushawishi na kupokea rushwa Sh. 300,000 kati ya Sh. 1,000,000 alizoomba kupewa.

Mbele ya Mahakama ya wilaya hiyo, Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Wakili Kelvine Murusuri, alidai mshtakiwa ambaye ni mwajiriwa wa Wakala wa Barabara (Tanroads) Mkoa wa Geita, akiwa na nia ovu, alishawishi kupewa Sh. milioni moja kutoka kwa Fabian Ngoni. Alidai lengo la kuomba hongo hiyo ni kumsaidia Ngoni ambaye ni mmiliki wa lori la linalobeba mchanga wa dhahabu lenye namba za usajili T 602 DLE ili asipime uzito kwenye mizani.

Wakili Murusuri alisema kuwa mnamo Machi 12, mwaka huu, mshtakiwa baada ya kushawishi kupewa kiasi hicho cha fedha, alifanikiwa kupewa Sh. 100,000 taslimu ikiwa ni malipo ya utangulizi kwa kuwa walikubaliana apewe Sh. milioni moja.

Alidai siku iliyofuata, yaani Machi 13, mshtakiwa alipokea Sh. 100,000 kwa njia ya M-Pesa kabla ya Takukuru kumwekea mtego uliomnasa baada ya kupokea tena Sh. 100,000 ndani ya gari lake lililopaki kwenye hoteli ya Mbalu iliyoko kwenye Mji Mdogo wa Katoro wilayani Geita.

Wakili Murusuri alidai kuwa mshtakiwa huyo alilifuatilia na kulikamata gari hilo ambalo lilikuwa kwenye barabara ambayo hapaswi kuisimamia.

Alidai mshtakiwa anakabiliwa na makosa matano yakiwamo ya kushawishi kupewa rushwa, kupokea rushwa ya fedha taslimu, kupokea rushwa kwa njia ya mtandano na kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu kinyume cha Kifungu Na. 302 cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2012.

Wakili Murusuri alidai upelelezi wa mashtaka hayo tayari umekashamilika, huku mshtakiwa akikana mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Gabriel Kurwijira.

Kesi hiyo itaendelea Aprili 25, mwaka huu, kwa ajili ya usikilizaji wa awali. Mshtakiwa aliachwa huru kwa dhamana baada ya kukidhi masharti yaliyowekwa dhidi yake.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akishiriki uteketezaji wa tani nane za nyama mbovu za nguruwe zilizokwisha muda wa matumizi zilizoingizwa nchini kinyume cha sheria eneo la Njiro jijini Arusha, juzi. Wengine ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo na Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichalwe, wakishuhudia tukio hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zaidi ya vyumba 1,000 vya madarasa vyahitajika

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, inakabiliwa na uhaba wa vyumba 1,350 vya madarasa katika shule za msingi na kusababisha changamoto kwa walimu na wanafunzi ya msongamano darasani na baadhi yao kusomea chini ya miti.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vyumba vitano vya madarasa vilivyojengwa katika shule za msingi za Mukarama ya Kata ya Rukoma na Bundaza ya Kata Nyakibimbili kwa ufadhili wa Shirika la World Vision Tanzania, Kanda ya Kagera, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa halmashauri hiyo na Kaimu Ofisa Elimu Msingi, Devotha Mtesigwa, alisema kuwa vinahitajika vyumba vya madarasa 2,350 na vilivyopo ni 1,010.

Mtesigwa alisema kuwa katika bajeti ya mwaka ya fedha 2019/2020, wamebajeti ujenzi wa vyumba 23 vya madarasa vyenye thamani ya Sh. milioni 460 ambavyo vikikamilika vitapunguza uhaba wa vyumba vya madarasa.

Makamu Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo, Deogratias Kashasha, alisema changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa itapungua endapo wananchi watahamasishwa kuchangia kwa hiari badala ya kutumia vitisho.

"Vikitumika vitisho kwa wananchi lengo linaweza lisitimie, wananchi wahamasishwe wakubali kutoa michango yao kwa hiari, hii itasaidia kupata michango, lakini pia kuepusha kuzuka kwa kero zinazoweza kusababisha wananchi kuichukia serikali yao," alisema.

Alisema, wananchi wakikaa pamoja na kujiongoza wenyewe kuchangia nguvu zao wanaweza kufanya kazi bora na kupunguza changamoto zilizopo za uhaba wa vyumba vya madarasa na miundombinu mingine na kuwa watakapofika wafadhili kuwasaidia wawakute wamejiandaa.

Akizungumza kwa niaba ya Meneja wa World Vision Kanda ya Kagera, Mratibu wa World Vision Ibwera, Lugembe Ng'oga, alisema vyumba hivyo vitano vya madarasa vimegharimu Sh. milioni 119.3.

Mmoja wa walimu wa Shule ya Msingi Mukarama, Julius Slivand, alisema kuwa wamekuwa wakipata shida kuwafundisha wanafunzi waliosongamana darasani maana hushindwa kuwafikia wanafunzi na kuwaeleza pale wanapokosea.

"Muda unakuta umekwisha wakati wanafunzi wote hawajaweza kuzungukiwa, inasababisha uelewa kuishia katikati au wanafunzi wengine wasielewe kabisa, hali hii inasababisha kushusha ufaulu wa watoto," alisema. Baadhi ya wanafunzi waliozungumza na Nipashe akiwamo Jovina Philimon, mwanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Bundaza, alisema msongamano darasani una athari nyingi ikiwamo kuandika vibaya, kuambukizana magonjwa kama mafua, kikohozi na kifua kikuu, na kutumia fursa hiyo kuwajengea madarasa ya kutosha ili kuepukana na changamoto hizo.

# Bil. 12/- zaongeza uzalishaji maziwa

**Na Dege Masoli,** TANGA

MKOPO wa Sh. bilioni 12 kwa ajili ya upanuzi wa kiwanda cha maziwa cha Tanga (Tanga Fresh), umeleta manufaa baada ya kukiongezea uwezo wa kuzalisha maziwa ya muda mrefu (Utra High Temperature) kutoka lita 50 hadi 120 kwa siku.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkoa ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, iliyosomwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela kwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, mkopo huo umeongeza uwezo wa kiwanda hicho kuzalisha.

Aidha, Shigela alieleza kuwa mafanikio hayo yameongeza pia ukubwa wa uhitaji wa maghafi na uzalishaji mdogo wa maziwa wa lita 70 kwa siku, umeshindwa kukidhi mahitaji ya kiwanda ya lita 120 na kuwa changamoto nyingine.

Hata hivyo, alieleza hatua ya upigaji chapa mifugo kuwa ng'ombe na punda wapatao 536,533, wamepitiwa kati ya lengo la upigaji chapa 503,545 sawa na asilimia 106.6 ya mifugo yote iliyopo Mkoa wa Tanga.

Akizungumzia changamoto hiyo, Shigela alisema imetokana na wafugaji wengi kutofuga kibiashara na kushindwa kumudu bei za pembejeo na huduma za mifugo na tija ndogo ya uzalishaji kutokana na aina ya mifugo na mifumo iliyopo ya uzalishaji wa mifugo.

"Asilimia 27 tu ya maziwa yanayozalishwa ndiyo hufikishwa kiwandani, asilimia 73 inatumiwa na wafugaji na walaji bila kusindikwa.

Ulaji wa mazao ya mifugo uko chini ya kiwango cha kitaifa na kimataifa," alieleza Shigela kwenye taarifa yake hiyo.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni upungufu wa wagani kwa asilimia 50 hasa kwa upande wa vijijini na uhaba wa nyenzo, malisho na maji hasa wakati wa kiangazi.

Kwa upande wa wizara hiyo, Shigela aliomba mkoa kusaidiwa uzalishaji wa mitamba 1,000 kwa kutumia dhana ya Private Public Partnership (PPP) kwa kushirikiana na taasisi za kiserikali zilizopo Tanga, ikiwamo mashamba yaliyopo nje ya mkoa.

Aliomba wizara kusaidia upatikanaji wa madume bora ya asili ya Bomani na Sahiwah ya India, Gir na Cerrralando ya kutoka Brazil ambayo huboresha uzalishaji wa maziwa na nyama.

Ulega kwa upande wake aliahidi kushirikiana na mkoa kuhakikisha kero zilizoainishwa kwenye taarifa hiyo zinapatiwa ufumbuzi ili kukiwezesha kiwanda hicho kufikia lengo na kuwa mkombozi kwa wafugaji.



Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa Tanzania Breweries Limited (TBL), Amanda Walter, akitoa mada katika semina kuhusu unywaji kistaarabu kwa askari wa Jeshi la Polisi kituo cha kati jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yawaonya wanaopotosha wavuvi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

OFISA Mfawidhi wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi Kanda ya Ziwa, Victory Mtambalike, amewaonya baadhi ya wavuvi walioanza kupotosha kauli ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kwamba serikali imeruhusu samaki aina ya sangara wenye ukubwa wa sentimita 85, kuanza kuvuliwa.

Kauli hiyo aliitoa baada ya siku chache tangu wadau wa sekta ya uvuvi, ukanda wa Ziwa Victoria wakutane na Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji, jijini Mwanza na kuwasilisha hoja 22 zinazolenga kuboresha sekta hiyo.

Aidha, serikali katika kikao hicho iliahidi kuzifanyia kazi ajenda hizo ikiwa pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria za Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009. "Zimesikika habari za kuwapo kwa baadhi ya wavuvi ndani ya Ziwa Victoria, walioanza kuhamasisha wenzao kwamba serikali imeruhusu samaki wenye zaidi ya ukubwa wa zaidi ya sentimita 85 wavuliwe, jambo ambalo sio sahihi bali ni uzushi wa watu kwa kutaka kujinufaisha wao kwa mashahi yao binafsi, kwa yeyote atakaye kamatwa anavua samaki hao hatutakuwa na simile," Mtambalike alisema.

Katika mkutano huo, Waziri Mpina, aliwaonya wenye viwanda vya kuchakata minofu ya samaki ambao wanaendelea kupunguza bei elekezi ya serikali ya Sh. 5,500 kwa kilo moja ya samaki. Naye msemaji wa Chama cha Wavuvi Tanzania, Sijaona James, aliwataka wavuvi kuwa na subira wakati serikali ikiendelea na mchakato wa mabadiliko ya sheria ambayo imekuwa ikitoa ukomo kwa wavuvi kuacha kuvua aina ya sangara mwenye ukubwa zaidi ya sentimita 85. Kilio cha wadau wa sekta ya uvuvi ni kwamba wateja wao wakubwa wa nchi za Hong Kong, Vetinam, China, Israel na Japani, wameanza kukimbilia masoko ya Uganda na Kenya, hali hiyo imesababisha viwanda vingi vya kuchakata minofu ya samaki vya nchini kushusha bei ya samaki na kushindwa kuzalisha kwa kiwango kinachostahili.

## Mganga wa jadi atuhumiwa mauaji ya watoto

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linamshikilia mganga wa jadi James Kapyela (52), pamoja na mtoto wake Michael Kapyela (14), kwa tuhuma za kuhusishwa na tukio la mauaji ya watoto wawili ambao maiti zao zilikutwa katika chumba anachotumia kutolea tiba.

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Mathias Nyangi, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa saba mchana, baada ya mtoto mmoja aliyekuwa amefungiwa ndani pamoja na marehemu hao wawili kutoroka na kwenda kutoa taarifa kwa wananchi.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo, watoto hao waliofahamika kwa jina la Nicolous Mwambage (7) na Emanuel Juma (4), walifariki dunia baada ya kufungiwa katika chumba ambacho Kapyela alikuwa akitumia kutolea tiba za jadi pia alikuwa amehifadhi gari bovu aina ya Chaser Saloon.

Imedaiwa kuwa wakati mganga huyo akiendelea kuwatibu watoto hao aliwaacha ndani ya chumba hicho na waliingia ndani ya gari hilo bovu na kujifungia kisha kushindwa kufungua milango na vioo kitendo kilichosababisha kukosa hewa.

Baada ya muda mrefu watoto wawili walifariki dunia na mmoja ambaye alikuwa ni watatu, alifanikiwa kutoka na kwenda kutoa taarifa ya vifo vya wenzake kwa majirani wanaoishi karibu na mganga huyo.

Majirani baada ya kupata taarifa hizo huku wakiwa na hasira, walivamia nyumba ya mganga huyo wa jadi na kuichoma moto pamoja na kuharibu mali zilizokuwamo nyumbani kwa mganga huyo.

Wakati tukio hilo likiendelea polisi walifika katika eneo la tukio na kumkamata mganga huyo na mtoto wake na kutuliza vurugu za wananchi waliokuwa wakiendelea kuchoma moto nyumba. Baada ya hali kuwa shwari Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, alifika katika eneo la tukio ili kuwaasa wananchi waliokuwa na hasira na kuliagiza Jeshi la Polisi kufanya msako wa waganga wa jadi wanaofanya shughuli zao mkoani humo bila kufuata taratibu. "Ninawaagiza polisi fanyeni msako ili kuwabaini watu wanaofanya shughuli za uganga wa jadi bila kusajiliwa, kuna sheria ambazo ni lazima zifuatwe ili mtu aweze kufanya kazi hiyo, si kila mtu kujifanyia, hivyo wakamateni wote ambao hawajasajiliwa ili sheria ifuate mkondo wake," Wangabo alisema.

Alisema kuwa iwapo mganga wa jadi atakuwa amesajiliwa itakuwa rahisi kufahamika anapofanyia shughuli zake na serikali kukagua maeneo yake anayofanyia kazi kwa ajili ya usalama wa wateja wake.

Mmoja wa wananchi ambao ni majirani wa mganga huyo wa jadi aliyejitambulisha kwa jina la Debora Maenge, alisema anasikitika kutokana na kuwa tukio hilo limetokea katika mtaa wao na kwamba mtuhumiwa ni jirani yao na siku zote wamekuwa wakijua ni mtu mwema.

# Upekuzi madini kuimarishwa kwa wachimbaji wadogo

**Na Mwandishi Wetu,** HANANG'

SERIKALI wilayani Hanang' imesema ipo macho kulinda rasilimali zake na itafanya hivyo kwa kuimarisha upekuzi kwa wachimbaji hadi maeneo nyeti ya maungo yao ili kuwabaini wanaokwepa kulipa kodi baada ya kupata dhahabu.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Hanang', Paul Bura, aliyasema hayo wakati wa kuapishwa kwa viongozi wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (Marema) Tawi la Bassotu mwishoni mwa wiki.

Eneo la Bassotu lina migodi ya wachimbaji wadogo wadogo wa dhahabu.

Aliwataka wachimbaji hao kutimiza haki na wajibu wao wanapokuwa wanachimba madini hayo kwa kuhakikisha wanalipa kodi na mrabaha wa serikali unaostahili.

Alisema pamoja na hayo, wanapaswa kupendana wakitambua kuwa pale haki yako inapoishia, ndiyo haki ya mwingine inapoanzia, hivyo hatarajii kuwapo kwa "sarakasi nyingine". Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Manyara, Joseph Kumburu, aliwataka wachimbaji hao kufuata masharti ya leseni za uchimbaji wa madini wakati wanapofanya kazi ya uchimbaji madini.

Alisema wenye leseni hawaruhusiwi kuchimba bila kukubaliana na wenye mashamba na kabla hawajaanza kuchimba wawe wameyaweka mazingira yao vizuri.

Makamu Mwenyekiti wa Marema, Money Yousuph, alisema kiapo kwa viongozi hao kinawakumbusha kutekeleza majukumu yao kwa vitendo na uaminifu.

Alisema serikali imeshatimiza wajibu wake, hivyo wachimbaji nao wanapaswa kutimiza sehemu yao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Katibu wa Marema mkoani Manyara, Kibwe Tariq, alisema viongozi hao wanapofanya shughuli zao wanapaswa kutoa haki kwa wanaowaongoza, huku wakishirikiana kwa ukaribu na kamati za usalama na usuluhishi migodini.

"Kiapo chenu kitakuwa hakina maana yoyote ikiwa mtakuwa mnafanya kazi zenu kwa upendeleo, huba, ubaguzi na rushwa bila kutenda haki kwani uongozi ni dhamana tu mliyopewa na wachimbaji wenzenu," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama, Afya na Mazingira Migodini wa Shirikisho la Wachimbaji Madini (Femata), Dk. Bernard Joseph, alisema walevi hawapaswi kuingia migodini ili kuepusha majanga. Dk. Joseph alisema elimu ya usalama, afya na mazingira itakuwa inatolewa kila wakati ili shughuli za uchimbaji madini ziwe zinafanyika kwa usalama bila madhara ya ajali au vifo.



Makamu Mwenyekiti wa chama cha wachimbaji madini Mkoa wa Manyara (Marema), Money Yousuph, akielezea majukumu ya viongozi wa Marema Tawi la Bassotu wilayani Hanang' baada ya viongozi hao kuapishwa juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wizara kuiwezesha Tari Selian kutoa elimu ya utafiti wa kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WIZARA ya Kilimo imeweka malengo ya kuiwezesha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Tari Selian ili iendelee kutoa elimu kuhusu utafiti inaofanya kwa lengo la kuwawezesha wakulima kulima kisasa.

Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, alitoa ahadi hiyo mbele ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Maji na Mifugo ilipotembelea taasisi hiyo kujionea shughuli zinazofanywa na changamoto zake.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo itaendelea kuviwezesha vituo vya utafiti nchini kuhakikisha vinatengewa bajeti ya kutosha ili vilete mabadiliko ya kilimo kwa wananchi. Alivitaka vituo vya utafiti kuhakikisha vinahaulisha utafiti vinaoufanya kwa wakulima ili kuleta tija na mwisho wa siku wakulima waishi katika kipato cha kati.

"Kuna haja pia ya kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha wakulima wanawezeshwa zana ndogondogo za kilimo ili kurahisisha shughuli za kilimo shambani zitakazowasaidia kutumia muda mchache na kulima kilimo chenye tija zaidi," alisema.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mahmood Mgimwa, alisema changamoto kubwa katika vituo vya utafiti nchini iko katika fedha ili watafiti wafanye utafiti maeneo mbalimbali kwa lengo la kupata mazao bora.

Mgimwa aliongeza kuwa changamoto ya fedha pia imekuwa ikichangia maarifa hayo ya utafiti kutowafikia wakulima, hivyo alishauri serikali kuongeza bajeti zaidi katika taasisi hizo ili kusaidia kazi hizo za utafiti kufanyika kwa ufanisi mkubwa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania ya Tari Selian, Dk. Joseph Ndunguru, alisema kituo hicho ni kati ya vituo 17 vya utafiti vilivyopo chini ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari).

Dk. Ndunguru alisema kituo hicho kimekuwa kikifanya utafiti katika kilimo cha mahindi, ngano, shairi na maharage na kimepata mafanikio makubwa kutokana na kuzalisha mbegu za mazao hayo ambazo zinahimili ukame na tayari zimeleta manufaa kwa wakulima. Aliongeza kuwa hadi sasa, zaidi ya wakulima 10,000 wamenufaika na mbegu za maharage zinazozalishwa kituoni hapo ambazo zina uwezo mkubwa wa kustahimili ukame.

## Wanaouzunguka Mlima Kilimanjaro washirikishwa utunzaji wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SHIRIKA la Kimataifa la Solidaridad limewashirikisha wadau wa mazingira, uhifadhi, kilimo na mifugo kutoka wilaya zinazozunguka Mlima Kilimanjaro kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ili kuendelea kulinda na kutunza mazingira ya mlima huo.

Meneja wa Programu kwa Mazingira Endelevu kutoka shirika hilo, Maria Sengelela, amesema uhifadhi wa mazingira ya Mlima Kilimanjaro unatakiwa kuwa endelevu kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho.

Alisema hayo katika mafunzo maalum ya kujengeana uwezo yaliyotolewa jijini hapa mwishoni mwa wiki baada ya kubaini kuwapo kwa changamoto za kibinadamu na za kiasili zinazohatarisha uhifadhi wa mazingira katika eneo lote linalozunguka mlima huo.

Alisema athari za mabadiliko ya tabia nchi zinaonekana wazi katika eneo hilo kama vile kukosa mvua za kutosha na hivyo kusababisha ukame unaoathiri kilimo, maeneo ya malisho na maji kwa mifugo, au kunyesha mvua nyingi kupita kiasi na kusababisha mafuriko yanayozoa mashamba, makazi na kuharibu miundombinu.

Alisema ingawa wananchi wengi wa maeneo yanayozunguka mlima huo ni waathirika wa mabadiliko hayo yanayotokana na uharibifu wa mazingira, wanawake na watoto ndiyo waathirika wakubwa zaidi.

Alisema katika kutekeleza azima ya uhifadhi wa mazingira ya Mlima Kilimanjaro, shirika hilo linashirikisha taasisi za umma na binafsi, makundi ya kijamii kupata uelewa wa ustawi wa mazingira ya mlima huo.

"Jamii nyingi zilizoko maeneo tunayotekeleza miradi zina utamaduni ambao mwanamke ndiye msimamizi mkuu wa familia... kwa mfano anasimamia watoto na pia anasimamia mifugo, na unakuta inapotokea janga mfano la ukame, huwa anapata changamoto kubwa kuhakikisha mahitaji yote yanapatikana," alisema.

Mchumi Mwandamizi kutoka Wilaya ya Longido, Ally Msangi, alisema mabadiliko ya tabia nchi yanaathiri mipango ya kiuchumi ya wakazi wa wilaya hiyo.

Shughuli kuu ya uchumi katika Wilaya ya Longido iliyoanzishwa rasmi mwaka 2006 na halmashauri yake kuanza kazi mwaka uliofuata, ni ufugaji. Kwa mujibu wa ripoti ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Frank Mwaisumbe, wafugaji ni asilimia 95 ya wakazi wa wilaya hiyo.

Mwanasheria kutoka Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Devotha Salukele, alisema pamoja na changamoto zilizopo, hatua iliyofikiwa ni kubwa na katika baadhi ya maeneo yapo mafanikio hasa kwa wanawake.

Alisema wananchi wengi mbali na kuelewa namna ya kutumia ardhi bila kuharibu mazingira, pia wameweza kupata hati za umiliki.

Meneja wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Enduiment (WMA) wilayani Longido, Peter Millanga, alisema wanaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu uhifadhi wa mazingira kwa kuwa wameshaanza kuona athari zake.

Alisema mabadiliko ya tabia nchi yanachangiwa na kasi ndogo ya usimamizi miradi ya uhifadhi inayotekelezwa katika maeneo mengi yanayozunguka mlima huo.

# Zaidi ya mangariba 30 waachana na ukeketaji

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MANGARIBA zaidi ya 30 waliokuwa wakifanya kazi ya kukeketa wasichana na watoto kwa usiri katika eneo la Arusha Chini, Wilaya ya Moshi, wameamua kuachana na kazi hiyo na kuungana na Shirika la kiraia la Tusonge kupambana kulifikia kundi kubwa zaidi la mangariba waliobaki.

Ukeketaji wa watoto wa kike, ni kitendo kinachotumika kuondoa kabisa au sehemu ya nje ya viungo vya uzazi na kusababisha maumivu mengine kwenye viungo vya uzazi kwa sababu ambazo si za kitabibu.

Uamuzi wa mangariba hao kuanza kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia na ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto kwa wenzao ambao hawajafikiwa, ulitangazwa jana na kiongozi mstaafu wa mangariba hao, Safina Samwel, wakati walipokutana katika mkutano wa hadhara wa kutoa elimu (caravan) Kijiji cha Masaini kilichopo Kata ya Arusha Chini.

"Kundi hili wote tumeshajua madhara ya mila hii ya ukeketaji, sasa ili kufanikisha vita ya kutokomeza ukeketaji ni lazima kwanza sisi mangariba ambao tulikuwa tukifanya kazi hii ya kimila, tushirikiane kuhakikisha kuwa tendo hili la kikatili linaloendelezwa kwa madai ya utamaduni linatokomezwa," alisema ngariba huyo.

Mratibu wa mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia na ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto kutoka Shirika la Tusonge, Joyce Kessy, akizungumza na mangariba hao alisema:

"Katika jamii nyingi za kiafrika, wanawake, watoto na watu wanaoishi na mahitaji maalumu wamekuwa wakipitia ukatili wa kijinsia na ukeketaji kutokana na mila, desturi kandamizi na ukosefu wa uelewa kwa jamii juu ya haki za makundi hayo." Aliyataja madhara yanayotokana na ukeketaji kuwa ni maumivu yasiyopungua, magonjwa ya kuambukiza mara kwa mara yanayoweza kusababisha utasa, mfadhaiko wa akili, kuwa na kumbukumbu mbaya, vifo vilivyopitiliza, kuharibu maumbile husika, kukosa hamu ya tendo la ndoa na kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua na pale anapokeketwa.

Mpaka sasa, shirika hilo limetengeneza vijana shupavu ambao watakuwa askari kanzu ndani ya kata hiyo watakaofuatilia mienendo ya vijana wanaorubuni watoto wa kike kimapenzi, mangariba wanaoendeleza shughuli ya tohara kwa watoto wa kike, matukio ya ukatili wa kijinsia, unyanyasaji wa kingono na vipigo kwa wanawake.

Pia katika mkutano huo, Joyce aliwashauri mangariba hao kuwasukuma wazee wa mila na makundi rika ya vijana wa jamii ya wafugaji wa Kimasai, kuruhusu watoto wa kike kuandikishwa shule, kuachana na utamaduni wa kuoza watoto wadogo, kuchumbia wasichana wenye umri chini ya miaka 18 na kuzuia mimba za utotoni ambazo zimesababisha wasichana wengi kukatisha ndoto zao.

Mradi huo wa miezi mitano, unalenga kutekeleza eneo mojawapo la Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto Tanzania (NPA), unaendeshwa na Tusonge kwa ufadhili wa Shirika la Foundation For the Civil Society.

Awali akizungumza katika mkutano huo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Arusha Chini (WEO), Emmanuel Mosha, alisema kikundi kazi cha vijana kilichoundwa kimepewa baraka na ofisi yake na kitazunguka vijiji vyote vya kata hiyo kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia.

Tusonge ni shirika lisilo la kiserikali linalofanya kazi na makundi ya pembezoni wakiwamo wanawake, watoto, vijana na watu wenye ulemavu likitoa kwao elimu ya ujasiriamali, haki za binadamu na kupiga vita mila na desturi potofu zinazosababisha ukatili wa kijinsia na ukeketaji.



Ngariba mstaafu wa Kata ya Arusha Chini, Moshi Vijijini, Safina Samwel, akifafanua jambo wakati akizungumza na mangariba wengine zaidi ya 30 walioungana na Shirika la Tusonge, kupinga mila ya ukeketaji inayoendelea katika jamii ya wafugaji. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mghwira azionya taasisi zinazokwamisha maendeleo

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amezinyooshea kidole, taasisi tano za umma anazodai kuwa zimekuwa chanzo cha kukwamisha mchakato wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya wafanyabiashara mkoani humo.

Mghwira aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, katika kikao maalumu cha kusikiliza kero za wafanyabiashara wa mkoa huo.

"Sitakubali serikali iendeele kupakwa matope kwa uzembe wa baadhi ya watendaji kwenye taasisi zilizopewa dhamana na serikali. Wasikilizeni wafanyabiashara, waelekezeni ili waweze kuzalisha kwa wakati na kuzalisha bidhaa bora zenye viwango vya kimataifa.

"Na nyinyi wafanyabiashara, hakikisheni mnauza bidhaa zenu kwa kulinganisha na wafanyabiashara wa mikoa mingine, kwa kuwa wateja wamekuwa wakilalamika kuwapo kwa upandishaji bei holela wa baadhi ya bidhaa."

Alizitaja taasisi hizo ambazo zinazotakiwa kujitathmini kutokana na kauli hiyo ni Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (Osha), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Alisema baada ya kuwasikiliza wafanyabiashara wadogo na wakubwa mkoani hapo, amegundua kwamba baadhi ya taasisi za umma zimekuwa kikwazo kwa maendeleo ya uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Kabla ya mkuu huyo wa mkoa kueleza masikitiko yake, Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara mkoani hapo, Raymond Mmasi, alisema sheria kandamizi na zinazokinzana katika taasisi za umma, ndizo zinazosababisha kukwama kwa biashara.

Baadhi ya wafanyabiashara wa mkoa huo akiwamo Exaud Makyao, alisema kama serikali inataka kuingia kwenye uchumi wa viwanda ni lazima wafanye mabadiliko ya sheria, tozo na faini kwenye taasisi kama NEMC, TRA, TBS, TFDA na OSHA.

"Watu hawa wanapofika katika biashara yako kwanza wanatumia lugha za vitisho, ubabe na hata kukufungia biashara. Jambo hili limekuwa likisababisha usumbufu mkubwa kwetu sisi wafanyabiashara na hata wateja ambao tunawahudumia," alisema Makyao.

Akijibu baadhi ya hoja zilizoelekezwa kwao, Mwakilishi wa OSHA, Frank Mwaikatale, alisema kazi yao ni kusimamia sheria zilizotungwa na Bunge, lakini alikiri kusikia malalamiko ya kuwapo kwa lugha za vitisho wakati wa ukaguzi na kuahidi hilo litafanyiwa kazi na wateja wao wataona mabadiliko makubwa.

Kwa upande wake, Meneja Msaidizi wa Idara ya Forodha ya Mamlaka ya Mapato (TRA), Edwin Twato, alisema amepokea rasmi kero za wafanyabiashara hao na kuahidi kwamba watakwenda kuzifanyia kazi na yatajitokeza mabadiliko makubwa katika mamlaka hiyo.

# BBL yakabidhi zawadi washindi wa 'Coke Studio kunywa ushinde'

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KAMPUNI ya Bonite Bottlers Ltd ya Moshi (BBL) inayozalisha vinywaji baridi jamii ya Coca-Cola, imekabidhi zawadi za seti ya televisheni 22 pamoja na zawadi nyingine za fedha taslimu kwa washindi wa promosheni ya 'Coke Studio, Kunywa na Ushinde' katika mikoa ya kibiashara ya Kilimanjaro, Arusha, Karatu, Babati na Singida.

Akizungumza katika hafla fupi ya kukabidhi zawadi hizo juzi, Meneja mauzo wa kampuni hiyo mkoa wa Arusha, Boniface Mwasi, alisema BBL imekuwa na utaratibu mzuri wa kurudisha sehemu ya faida yake kwa wateja ambao wanaiunga mkono katika biashara ya soda jamii ya Coca Cola.

"Hii ni nafasi pekee kwa mteja kushinda zawadi kubwa kwa Sh. 500 na Sh. 1,000. Shindano linakwenda vizuri, tuna washindi kama 15,000 ambao wamejishindia zawadi mbalimbali na ambazo tumezitoa leo (juzi) ni televisheni 22, soda za bure zenye zawadi ya Sh. 5,000 na Sh. 10,000 ambazo zinatolewa papo hapo," alisema Mwasi.

Zaidi aliongeza: "Niseme tu kwa ujumla wake kwamba kumekuwa na hamasa kubwa kwenye hili Shindano la Coke Studio, Kunywa na Ushinde; na washindi wanaendelea kupatikana na inaonekana tunashinda kila kona ambayo tunafanya biashara maana tunapokea washindi sehemu zote ambazo Bonite tunafanya biashara. Soda jamii ya Coca Cola, Fanta, Sprite katika ujazo wa milimita 350 na milimita 500 zote zina zawadi."

Februari 14, mwaka huu, kampuni hiyo ilitangaza wiki 12 za Promosheni ya Coke Studio Afrika ya mwaka 2019 kwa wateja wake kunufaika na zawadi mbalimbali ikiwamo fedha taslimu hadi Sh. 100,000 na seti ya televisheni ya inchi 32.

Meneja Mkuu wa Mauzo na Masoko wa BBL, Christopher Loiruk, alinukuliwa akisema wakati wa uzinduzi wa promosheni hiyo, "Kuanzia Februari 15, mpaka Aprili 26, mwaka huu, tutaendesha promosheni kabambe ambapo wateja wetu kila watakaponunua soda ya Coca Cola, Fanta zote pamoja na Sprite watapata fursa ya kuweza kujishindia zawadi zetu mbalimbali," alisema.

Alizitaja zawadi za mwaka huu zitakazotolewa na Bonite Bottlers Ltd kuwa ni seti ya televisheni ya inchi 32, pesa taslimu kuanzia Sh.5, 000 hadi Sh. 100,000.

Kwa mujibu wa Loiruk, promosheni hiyo ya Coke Studio itawapa wateja wake fursa ya kujishindia pia vinywaji vya bure kila wanaponunua soda za Bonite Bottlers.

Hivi sasa, maonyesho mbalimbali ya Coke Studio Afrika yanaendelea kufanyika kupitia runinga ya East Africa Televisheni (EATV).

Nipashe
Spotika
NIPASHE JUMATATU MACHI 25, 2019



SIMBA, TP MAZEMBE MECHI YA KISASI CAF UK.15

# HEKAHEKA...



## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Eden Hazard, jana ametimiza mechi 100 akiwa na timu ya Taifa ya Ubelgiji wakati wakiivaa Cyprus kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020. Kwa mara ya kwanza Hazard kuichezea timu hiyo ilikuwa miaka 10 iliyopita, mnamo Novemba 2008 wakati huo akiitumikia klabu ya Lille.

Beki wa England, Michael Keane (mbele), katika hehaheka za kumzuia mshambuliaji wa Jamhuri ya Czech, Patrik Schick, kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Wembley juzi na wenyeji kushinda 5-0. **PICHA: MTANDAO**

# WA5 WAKUSAJILIWA NA ZIDANE MADRID

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane ameanza kipindi cha pili cha kuwa kocha wa Real Madrid, huku akianza kwa kumsajili beki wa kimataifa wa Brazil, Eder Militao kutoka kwa miamba wa Ureno, FC Porto kwa ada iliyotajwa kuwa ni pauni milioni 43 kwa mkataba wa miaka sita.

Raia huyo wa Ufaransa ameonyesha wazi kwamba miamba hao wa Hispania walikuwa na tatizo kubwa kwenye safu ya ulinzi msimu huu na kujikuta wakiwa nafasi ya tatu kwenye msimamo wa La Liga, wakipitwa pointi 12 na wapinzani wao Barcelona ambao wapo kileleni mwa msimamo.

'Los Blancos' hao walijikuta wakiadabishwa kwenye hatua ya mtoano ya timu 16 katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ajax, kitu kilichoonyesha wazi kuwa kunatakiwa mrithi wa Sergio Ramos wakati atakapostaafu. Kukosekana kwake kukamfanya Dusan Tadic kuiwezesha Ajax kufunga mabao manne dhidi ya Real Madrid ambao ni mabingwa mara 13 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Militao amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa mabeki bora Ulaya tangu alipojiunga na FC Porto na amekuwa mhimili muhimu kwa Wareno hao wakati wakifuzu hatua ya robo fainali.

Usajili wa Militao ni kama mapinduzi mazuri kwa Los Blancos, kwani pia alikuwa akiwaniwa na timu kama Manchester United, PSG na Liverpool. Imeripotiwa kwamba Zidane amepewa pauni milioni 300 kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chake kipindi cha majira ya joto. Hii ina maana kwamba kuna wachezaji wengi ambao watatua hapo.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao Zinedine Zidane anaweza kuwasajili kipindi cha majira ya joto...

**5. Christian Eriksen**

Christian Eriksen amejiimarisha kama mmoja wa kiungo mshambuliaji bora Ulaya tangu alipojiunga na Tottenham Hotspur akiwa kijana akitokea Ajax Amsterdam mwaka 2013. Amefunga mabao 49 na kutoa pasi za mwisho 39 kwa kipindi cha miaka saba aliyokaa kwenye Ligi Kuu ya England.

Suala la ubunifu kwenye kiungo ya Real Madrid halijawa vizuri msimu huu, hivyo kuna mahitaji ya kuwa na kiungo mwingine zaidi kwenye akili kama Christian Eriksen. Yeye anaweza kuwa msaada mkubwa kwa Zidane msimu ujao kwani ameonyesha kiwango chake kizuri pale Tottenham.

Mkataba wa Eriksen pale White Hart Lane unaelekea mwisho, hivyo ni wakati mzuri kwake kutua pale Bernabeu.

**4. Mauro Icardi**

Icardi pengine anakaribia kumaliza muda wake na Inter Milan baada ya kuwa na matatizo na uongozi wa timu hiyo, hali iliyompelekea kuvuliwa kitambaa cha unahodha na kwa hivi sasa haichezei klabu hiyo licha yakuwa yuko fiti.

Matamshi ya kocha Luciano Spalleti baada ya ushindi dhidi ya AC Milan kwamba, Lautaro anaweza kumaliza tatizo la ushambuliaji la Inter, inamaanisha kwamba, kuna matumaini madogo zaidi kwa Icardi kubakia katika timu hiyo.

Raia huyo wa Argentina alijiunga na Inter Milan akiwa kijana na baadaye akaweza kujijenga mwenyewe kama mmoja wa wachezaji bora kabisa Ulaya na Ligi Kuu ya Italia. Ameifungia timu hiyo mabao 122 katika mechi 210 alizoichezea.

Kabla ya kuwekwa benchi, Icardi alikuwa ameshafunga mabao tisa katika mechi 20 za Ligi Kuu akiwa na Inter Milan msimu huu na kukosekana kwake kumewafanya 'Nerazzurri' hao kutupwa nje ya michuano ya Ligi ya Europa hatua ya 16.

Katika umri wake wa miaka 26, Icardi yupo kwenye kilele cha kipaji chake, kwa kuwa anaweza kuwa mrithi mzuri zaidi wa Karim Benzema. Na kutokana na matatizo yake ya sasa na Inter Milan, ana nafasi kubwa zaidi ya kutua pale Real Madrid.

**3. Paul Pogba**

Paul Pogba kwa sasa anaonyesha kipaji chake cha hali ya juu pale Manchester United baada ya kusajiliwa kwa mara ya pili kutoka Juventus. Kuteuliwa kwa Olé Gunnar Solskjaer kuwa kocha wa muda Manchester United kumekuwa na ishara chanya zaidi kwa Mfaransa huyo ambaye alionekana kushuka kiwango chini ya kocha Jose Mourinho msimu uliopita.

Pogba kwa sasa anafurahia kucheza, kwa kuwa amefunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho tisa kwenye Ligi Kuu ya England. Kumekuwa na uvumi kwamba, kiungo huyo wa Ufaransa anaweza kuondoka pale Manchester United kama watashindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

Mashetani Wekundu hao wana kazi kubwa ya kufuzu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kwani wapo nafasi ya tano katika msimamo, wakiwa wamepitwa pointi mbili na Arsenal inayoshika nafasi ya nne, huku mechi nane zikibakia kabla ya kumalizika kwa ligi hiyo. Wakishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, kutawafanya wafuzu moja kwa moja, lakini kwa sasa wanakabiliwa na mchezo mgumu dhidi ya Barcelona kwenye hatua ya robo fainali.

Real Madrid wana uhitaji mkubwa wa kiungo aina ya Paul Pogba ambaye anaweza kuwa mtatuzi wa matatizo yao.

**2. Kylian Mbappe**

Mbappe anaendelea kuonyesha kiwango chake cha hali ya juu baada ya kuisaidia Ufaransa kushinda taji la Kombe la Dunia nchini Urusi mwaka jana. Amefunga mabao 31 katika mechi 35 alizoichezea PSG kwenye mashindano yote msimu huu.

Mfaransa huyo kijana ameonyesha kumpiku mchezaji ghali zaidi Neymar msimu huu akiiongoza kwenye ufungaji wa mabao katika Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, akiwa na mabao 26.

Real Madrid tangu kuondokewa na Cristiano Ronaldo aliyetimkia kule Juventus kipindi cha majira ya joto kilichopita, wamekuwa na tatizo kubwa zaidi la ufungaji. Lakini Mbappe anaweza kuwa mrithi mzuri zaidi wa mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or.

Katika umri wake wa miaka 20, Mbappe anaweza kuisaidia zaidi Real Madrid kwa kipindi cha miaka mingi.

**1. Eden Hazard**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ubelgji amekuwa na kiwango cha juu zaidi pale Chelsea msimu huu, licha ya 'Blues' hao kuwa kwenye wakati mgumu Ligi Kuu. Ameifungia mabao 13 na kutoa pasi za mwisho 11 kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

Hazard ameshabainisha wazi kwamba angependa kucheza chini ya kocha Zinedine Zidane akimwelezea kama mmoja wa wachezaji waliomvutia zaidi kuingia kwenye soka wakati akikua.

Real Madrid imekuwa ikimfutilia mchezaji huyo kwa muda na uwapo wa Zidane sasa unaweza kumfanya Eden Hazard kuwa kwenye wakati mzuri zaidi wa kutua hapo katika dimba la Bernabeu kipindi cha majira ya joto kijacho.

Ujio wa Eden Hazard hapo Real Madrid unaweza kuiimarisha zaidi safu ya ushambuliaji ya Madrid na kuirudisha kwenye chati yake katika Ligi Kuu ya Hispania, La Liga. Kwa namna yoyote, Hazard anahitajika zaidi hapo Santiago Barnabeu.




Mbappe

**JE, WAJUA?**

ENGLAND haijapoteza mechi yoyote ya kufuzu kati ya 40 zilizopita za (Euro na Kombe la Dunia), ikiwa imeshinda mechi 31 na kutoka sare tisa tangu ilipofungwa bao 1-0 na Ukraine Oktoba 2009.



# MICHEZO

## NJE YA UWANJA



### BURUNDI YAMKOSESHA AUBAMEYANG AFCON 2019

**BUJUMURA,** Burundi

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, ambaye anaongoza kwa utupiaji mabao katika klabu hiyo ameshindwa kuisaidia timu yake ya Taifa ya Gabon kufuzu michuano ya fainali za Mataifa ya Afrika baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Burundi mjini Bujumbura juzi.

Gabon imemaliza nafasi ya tatu katika Kundi lao la C, ikiwa pointi mbili nyuma ya Burundi iliyoshika nafasi ya pili nyuma ya vinara Mali.

Kwa matokeo hayo Burundi imefuzu kwa mara ya kwanza kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika shukrani kwa kutoka sare ya bao 1-1 juzi, dhidi ya Gabon, ambayo imezikosa fainali hizo zitakazofanyika nchini Misri Juni mwaka huu.

Burundi ilifanya vizuri katika safu yake ya ulinzi, kabla ya kupata bao la kuongoza dakika ya 77 wakati Cedric Amissi alipoziona nyavu.

Hata hivyo, bao la kujifunga la Omar Ngando liliwawezesha Gabon kupata sare hiyo ya bao 1-1, lakini halikuweza kuwasaidia kufuzu.

Burundi sasa itajiunga na Mali iliyomaliza Kundi C ikiwa kileleni na pointi zake 14 kucheza fainali hizo zitakazofanyika Juni hadi Julai nchini Misri, huku Aubameyang na Gabon yake wakibaki kuwa watazamaji mwaka huu.



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatuos Chama, akifanya vitu vyake uwanjani. Mabao ya dakika za mwisho ya raia huyu wa Zambia ndiyo yaliyoifanya Simba kutinga hatua ya makundi dhidi ya Nkana FC ya Zambia na pia hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya AS Vita ya DR Congo.

# SIMBA, TP MAZEMBE MECHI YA KISASI CAF

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara Simba, wamepangwa kucheza dhidi ya TP Mazembe kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mechi ambayo itakuwa ni ya kisasi cha mwaka 2011.

Kwenye droo iliyofanyika Jumatano iliyopita, Simba ilipangwa dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, mechi ya kwanza ilipangwa kuchezwa mwezi ujao Aprili 5, Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na ya pili ikichezwa nchini DR Congo Aprili 12, mwaka huu.

Mwaka 2011 timu hizo zilipambana kwenye Ligi ya Mabingwa hatua ya raundi ya kwanza.

Matokeo ya mechi mbili za nyumbani na ugenini, pamoja na tukio lingine lililojitokeza ndicho kitakachosababisha mechi hiyo kuwa tamu na yenye ushindani wa hali ya juu, ukiachilia mbali kila timu kutaka kutinga hatua ya nusu fainali.

**Simba ilichapwa mabao 3-1 ugenini**

Ilikuwa ni mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa, baada ya Simba kuitoa Elan Club Mitsudje ya Comoro kwenye mechi ya awali kwa jumla ya mabao 4-2 jijini Dar es Salaam, baada ya suluhu ya bila kufungana ugenini.

Mechi hiyo ilichezwa Machi 20, Lubumbashi nchini Congo DR na Simba ikachapwa mabao 3-1. Mabao ya TP Mazembe yaliwekwa wavuni na Patou Kabangu dakika ya 12, Narcisse Ekanga dakika ya 21 na Alain Dioko Kaluyituka dakika ya 64, huku la kufutia machozi la Simba likifungwa na Emmanuel Okwi dakika ya 76 kwa mkwaju wa penalti.

Ina maana kuwa kwenye mechi ya robo fainali, mchezaji pekee wa Simba aliyekuwapo kwenye kikosi kilichocheza na TP Mazembe mwaka 2011 ni Okwi pekee.

**Ikachapwa tena nyumbani mabao 3-2**

Mechi ya marudiano ilichezwa Aprili 3, 2011, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na Simba ikachapwa mabao 3-2 na kuondolewa kwenye raundi ya kwanza kwa jumla ya mabao 6-3.

Kwa upande wa washindi, mabao yao yalifungwa na Given Singuluma la kwanza dakika ya 17 na Alain Kaluyituka akifunga mabao mawili dakika ya 64 na 72.

Na yale ya Simba yalifungwa na Shija Mkina dakika ya 58 na Mbwana Samatta dakika ya 65.

**Soka fitina ikaiondoa TP Mazembe Caf**

Mara baada ya kufungwa mechi hizo, Simba ilikata rufani Shirikisho la Soka Afrika (Caf) kulalamikia kitendo cha TP Mazembe kumchezesha mchezaji Janvier Besala Bokungu ambaye hakuhamishwa kihalali kutoka Esperance ya Tunisia.

Caf walithibitisha kuwa ni kweli na Simba ikapewa ushindi, TP Mazembe ikiondolewa kwenye michuano hiyo.

Baadaye Bokungu alikuja kujiunga na Simba mwaka 2015 na kucheza kwa misimu miwili.

Baada ya kurejeshwa kwenye raundi ya pili ya Ligi ya Mabingwa Simba ikapangwa kukutana na Wydad Casablaca kwenye hatua hiyo, ambayo kama ingeshinda ingetinga moja kwenye moja kwenye hatua ya makundi.

Hata hivyo, kisicho riziki hakiliki, Simba ikabugizwa mabao 3-0 kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Uhuru, Mei 28, 2011.

Simba ilizuia hadi dakika ya 87 na ilionekana kama timu hizo zingekwenda kwenye mikwaju ya penalti, lakini Fabrice N'Guessi Ondama alianza kufunga bao dakika ya 87, Ayoub El Khaliqi dakika tatu za nyongeza na Mouhcine Lajour kwenye dakika ya sita ya nyongeza.

Simba ilitolewa na kushushwa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho.

Kutokana na matukio yote hayo, mechi hiyo itakuwa ya kisasi kwa kuwa Simba itataka kulipa kisasi cha kufungwa mwaka 2011, TP Mazembe ikiwa na hasira ya kupokonywa ushindi wa uwanjani mwaka huu.

## NUKUU


“Kwa mchezaji kama [Kylian] Mbappe wakati unapozungumza kuhusu mustakabali wa baadaye, huhitaji kusema atakavyokuwa muda wa miaka mitano ijayo, kwa kipindi cha miaka 10. Yeye ni wa ajabu kabisa, nadhani ukigeukia umri wake [na kuzingatia] umri wa Cristiano [Ronaldo], wa [Lionel] Messi, wote ni zaidi ya miaka 30, Neymar ana miaka 27... wakati unakwenda sokoni kiwango na umri pia ni kigezo, nadhani ni mchezaji mwenye thamani zaidi duniani, katika uhamisho wa kufikiri, yeye ni mchezaji ghali sana katika soka kwa sasa,” **Jose Mourinho aliiambia beIN Sports.**




“Wakati nilipokuwa mdogo, niliipenda United. Ninaapa. Kama mtoto mdogo, niliipenda United. Ukweli ninawapenda. Na ninataka kulionyesha hili na kuwaletea watu furaha kwa sababu, ni wazi, ninataka kushinda. Ninataka kuendelea kuonyesha mapenzi yangu kwa mpira. Ninajua nini ninachoweza kukifanya. Nina imani ndani ya uwezo wangu. United ni klabu muhimu, na si England pekee bali katika ngazi ya dunia na ningependa kusaidia kuleta kombe kwa mashabiki,” **Alexis Sanchez.**





“Kila kitu kinachotokea kinahukumiwa na zama za [Sir Alex] Ferguson wanasema eti laiti Ferguson angekuwapo hapa, hali hii isingeweza kutokea, Ferguson hakutaka kufanya hivyo kama hiyo. Ferguson angefanya hivyo kama hii. Kila kitu kilikuwa Ferguson. Ikiwa ni mimi, ningesema simjui Ferguson tena. Na mimi kuja hapa na nataka kufanya historia yangu mwenyewe, nataka kufanya hadithi yangu mwenyewe, kwa hivyo sitaki kusikia kilichotokea hapo awali. Ninataka kufanya hivyo kwa sasa nakuja na mawazo mapya,” **Zlatan Ibrahimovic alisema akiliambia Gazeti la The Mirror.**







Aguero


Kane


Tadic


Marega


Lewandowski


Messi

# Ronaldo anayatafuta kwa tochi mabao yao Uefa

**LONDON,** England

MSIMU wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa 2018/2019, unaelekea mwisho wakati sasa ikiwa kwenye robo fainali.

Mabao yamekuwa muhimu zaidi kwa klabu kuiwezesha kufika kwenye hatua hiyo. Bila mabao hayo klabu hizo zingeondolewa muda mrefu, lakini kwa kutegemea wafungaji mabao mambo yamekuwa tofauti.

Likija suala la wafungaji mabao, sio wengi wameweza kuwa kwenye kiwango kisichoshuka cha ufungaji kuliko Cristiano Ronaldo kwa miaka kadhaa, huku Mreno huyo akiwa kwenye kiwango cha juu zaidi katika mashindano hayo.

Huku akiwa na mabao 125 katika mechi 166 alizocheza, yeye ni mfungaji bora wa wakati wote kwenye historia ya michuano hiyo, akiwa pia ameshinda Kiatu cha Dhahabu cha ufungaji bora katika kila msimu kwa kipindi cha misimu sita iliyopita.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 34, mabao yake matatu ‘hat-trick’ aliyofunga kwenye mchezo wake wa mwisho yalipindua matokeo na kuiondoa Atletico Madrid.

Lakini pamoja na mabao yake hayo kuiwezesha Juventus kutinga robo fainali ya michuano hiyo, mchezaji huyo anayevaa jezi namba saba msimu huu hayupo katika orodha ya wafungaji bora kwenye michuano hiyo.

Kwani Ronaldo ‘hat-trick’ yake hiyo ilimfanya kufikisha mabao manne kwenye michuano hiyo msimu huu.

Hapa tunawaangalia wachezaji 10 ambao wanaongoza kwa ufungaji mabao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

**10. Paulo Dybala (Juve) - Mabao 5**

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 25, kwa muda mrefu amekuwa mchezaji muhimu zaidi kwa timu ya Juventus kwenye safu ya ushambuliaji. Hata hivyo, tangu kuwasili kwa Ronaldo kipindi cha majira ya joto kilichopita inaonyesha mambo ni kama yamebadilika.

Dybala alikuwa nyota, lakini sasa hajawa kwenye kiwango kile cha mwanzo, lakini pamoja na yote hadi sasa mchezaji huyo amefunga mabao matano na kuisaidia Juventus kuendelea kutafuta taji hilo kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 22.

**9. Sergio Aguero (Man City) - Mabao 5**

Manchester City inaweza kuwa kwenye wakati mzuri zaidi kwenye Ligi Kuu nchini England, lakini bado hawajawa na nguvu kubwa kwenye michuano ya Ulaya.

Lakini sasa Man City wanajipanga kushinda taji hilo kwa mara ya kwanza, huku mshambuliaji wake Sergio Aguero akionekana kuwa msaada mkubwa zaidi kwa msimu huu.

Mchezaj huyo mwenye umri wa miaka 31 raia wa Argentina, amefunga mabao matano msimu huu katika mechi tano alizocheza, yakiwamo mabao mawili aliyofunga dhidi ya Schalke 04 na sasa City wapo kwenye nafasi nzuri ya kuliwania taji hili kwa mara ya kwanza.

**8. Harry Kane (Tottenham) - Mabao 5**

Ni mmoja wa washambuliaji bora duniani kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Harry Kane amekuwa hana ajizi akiwa kwenye eneo la goli na amekuwa msaada mkubwa kwa Tottenham.

Hadi sasa msimu huu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ni mshindi wa Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora katika michuano ya Kombe la Dunia iliyopita. Kwa sasa ana mabao matano katika mechi saba alizoichezea Spurs na ameisaidia klabu hiyo kutinga hatua ya robo fainali na sasa wanataka kutinga nusu fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza. Harry Kane ndiye mhimili mkuu wa ufungaji mabao kwa timu hiyo.

**7. Andrej Kamaric (Hoffenheim) - Mabao 5**

Ingawa Hoffenheim haijafika mbali kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu ikiwa imeondolewa hatua ya makundi, lakini Wajerumani hao walikuwa na kiwango cha kuvutia.

Kazi kubwa aliifanya Andrej Kramaric mwenye umri wa miaka 27 raia wa Croatia, akiwa ametikisa nyavu mara tano na kutoa pasi ya bao moja.

**6. Neymar Jr (PSG) - Mabao 5**

Neymar amejikuta mwenyewe katika nafasi ya sita katika orodha ya wafungaji bora wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, ingawa kwa mara ya mwisho alicheza kwenye michuano hiyo Desemba mwaka jana.

Majeraha yalimfanya kuwa nje ya dimba msimu uliopita na kuukosa mchezo dhidi ya Manchester United wa raundi ya mwisho, na ameshuhudia timu yake ikiondolewa kwenye mashindano hayo.

Pamoja na PSG kukosa huduma ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, lakini ameweza kufunga mabao matano katika mechi sita alizoichezea timu hiyo, huku moja akifunga dhidi ya Red Star Belgrade.

**5. Edin Dzeko (AS Roma) - Mabao 5**

Edin Dzeko kwa urahisi tu ni mmoja wa wachambuliaji ambao huwa hawapewi nafasi kubwa. Lakini mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 32, amekuwa mmaliziaji mzuri tu na ana rekodi nzuri ya kufunga mabao.

Msimu huu raia huyo wa Bosnia amefunga mabao matano na kusaidia pasi za mwisho nne katika mechi sita alizocheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, ingawa alishuhudia Roma ikitolewa na Porto.

**4. Moussa Marega (Porto) - Mabao 6**

Moussa Marega amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa kikosi chake msimu huu na ameisaidia Porto kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo raia wa Mali amefunga mabao hayo sita katika mechi sita alizoichezea timu yake.

**3. Dusan Tadic (Ajax) - Mabao 6**

Dusan Tadic alisajiliwa na miamba wa Uholanzi, Ajax kipindi cha majira ya joto kwa kitita cha euro milioni 11.4.

Hadi sasa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amekuwa kwenye kiwango kizuri zaidi katika timu yake ya Ajax, akifunga mabao sita na alikuwa mmoja wa wachezaji walioiangamiza Real Madrid kwenye mchezo wa raundi ya mwisho.

**2. Robert Lewandowski (Bayern) - Mabao 8**

Robert Lewandowski alijitengenezea jina lake mwenyewe katika jezi za Borussia Dortmund, akiisaidia klabu yake kushinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga pamoja na kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2013.

Hata hivyo, miamba wa Ujerumani, Bayern Munich waliipata saini yake na lengo kubwa likiwa ni kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 30, amekuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu huu akifunga mabao nane katika mechi nane alizoichezea Bayern Munich, ingawa kwa sasa imetolewa kwenye michuano hiyo na Liverpool.

**1. Lionel Messi (Barca) - Mabao 8**

Barcelona ni washindi mara tano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na ikishinda mataji matatu mara mbili kwa msimu, lakini wamekuwa kwenye wakati mgumu katika miaka ya hivi karibuni.

Hata hivyo, ‘Blaugrana’ hao wana mchezaji bora wa wakati wote akiwa na umri wa miaka 31, na msimu huu alipambanua mwenyewe kwamba lengo lake kubwa ni kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kulipeleka pale katika dimba la Camp Nou.

Lionel Messi alianza msimu huu kwa staili ya aina yake wakati alipofunga ‘hat-trick’ kwenye ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya PSV na tangu hapo ameendelea kuwa kwenye kiwango cha juu zaidi.

Hadi sasa msimu huu, mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina amefunga mabao nane na kutoa pasi za mwisho nne kwenye michezo mitano aliyoshuka dimbani.

Akiwa ameingia na mpinzani wake Ronaldo ambaye aliiondoa Atletico Madrid, Lionel Messi, alimjibu kwa kufunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho mbili wakati wakiifunga Lyon mabao 5-1 na kuiondoa kwenye michuano hiyo ya Ulaya msimu huu. Na ni wazi kwamba msimu huu wana nafasi kubwa zaidi ya kulibeba taji hilo.

## Michezo



Straika wa Yanga, Heritier Makambo (kulia) na mwenzake, Ibrahim Ajibu, wakishangilia moja ya mabao yao kwenye Ligi Kuu.

# UTAMU NA UCHUNGU LIGI KUU BARA KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

HII ni wiki ambayo Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha mechi za kufuzu Afcon zinazotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu nchini Misri.

Ligi hiyo imeanza kuelekea ukingoni, huku baadhi ya timu zikiutafuta ubingwa kwa udi na uvumba, zingine zikitaka kujiongezea pointi ili zibaki salama kwenye Ligi Kuu, lakini zipo zinazopigana kufa au kupona kuondoka kwenye hatari ya kushuka daraja.

Mbali na hilo kuna vita nyingine ya kuwania Kiatu cha Dhahabu na rekodi nyingi nyinginezo. Itaendelea baada ya mechi za mwisho za Afcon.

Mwandishi wa makala haya amekusanya kumbukumbu, takwimu na rekodi mbalimbali zilizopo mpaka sasa ambazo zimewekwa kwa mtindo wa namba...

**559-** Hii ni idadi ya ya mabao yote yaliyofungwa mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilisimama wiki iliyopita kupisha mechi za Afcon.

**296-** Hizi ndiyo idadi ya mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo zimeshachezwa mpaka sasa.

**202-** Namba hii inasimama kuwa ndiyo idadi ya wachezaji waliofunga mabao yote 559 ya Ligi Kuu ambayo yamepachikwa wavuni mpaka sasa.

**76-** Haya ni mabao yaliyofungwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, ikiwa ndiyo uwanja ulioruhusu nyavu zake kutikiswa mara nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**67-** Hizi ni idadi ya pointi za kinara anayeongoza Ligi Kuu ya Tanzania ambaye ni Yanga akiwa juu ya Azam FC kwa tofauti ya pointi nane.

**59-** Hii ni idadi ya mabao yaliyofungwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam ambao ni uwanja wa nyumbani wa timu za African Lyon ikicheza na timu zote kasoro Simba na Yanga, KMC ya Kinondoni pia hutumia uwanja huo kama wake wa nyumbani.

**46-** Ni mabao yaliyofungwa na Azam FC kwenye Ligi Kuu, ikiwa inaongoza kwa kupachika mabao mengi hadi sasa.

**45-** Ni idadi ya mabao ambayo timu kongwe na watani wa jadi hapa nchini, Simba na Yanga zimepachika nyavuni kila moja. Simba imepachika idadi hiyo ikiwa na pungufu ya michezo sita nyuma ya hasimu wake.

**40-** Namba hii inasimama kama idadi ya mabao ya kufungwa ya Stand United. Imefungwa idadi hii ya na kuwa timu iliyoruhusu nyavu zake kutikiswa mara nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu hadi sasa.

**39-** Ni mabao yaliyofungwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, ambao ni wa nyumbani wa Azam FC.

**36-** Hizi ni idadi ya penalti zote zilizotolewa na waamuzi kwenye Ligi Kuu mpaka kufikia sasa, ambapo mechi 296 zimeshachezwa. Namba hii pia inasimama kama pointi za timu tano kwenye Ligi Kuu ambazo zinawiana kwa pointi, huku zikipishana tu kwa mabao ya kufunga na kufungwa. Timu zenye idadi hiyo ya pointi ni Mwadui, Kagera Sugar, JKT Tanzania, Mbao FC na Stand United.

**30-** Biashara United ya Mara ina idadi ya pointi hizi kwenye Ligi Kuu.

**31-** Hii ni idadi ya mabao ya penalti yaliyofungwa kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**29-** Timu ya Stand United imefungwa idadi hii ya mabao kwenye Ligi Kuu.

**22-** African Lyon inamiliki idadi hii ya pointi, ikiwa ni chache kuliko timu nyingine 19 zinazoshiriki Ligi Kuu. Kadhalika, ni idadi ya wachezaji waliofunga mabao kwa mikwaju ya penalti. Ingawa penalti zilizofungwa ni 31, lakini kuna wachezaji wamefunga zaidi ya penalti moja, wengine mbili mpaka tatu kwenye mechi tofauti.

**21-** Ni idadi ya mechi ambayo Yanga imeshinda na kuwa ndiyo timu iliyoshinda mechi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa. Lakini hii pia ni idadi ya michezo ambayo Simba imecheza mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, ikiwa ndiyo timu iliyocheza mechi chache zaidi.

**18-** Ni mabao ambayo kinara wa Ligi Kuu, Yanga imefungwa kwenye hadi sasa.

**17-** African Lyon ndiyo timu iliyopoteza mechi nyingi zaidi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu. Namba hii inasimama kuwa ni idadi ya mechi ilizochapwa.

**16-** Haya ni mabao yaliyofungwa na straika Salum Aiyee wa Mwadui ambaye ameendelea kuwa kinara wa kucheka na nyavu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi leo.

**14-** Coastal Union ya Tanga na KMC ya Kinondoni ndiyo timu zilizota sare nyingi kwenye Ligi Kuu kila mmoja mpaka sasa. Hii ni idadi ya sare ambazo imezipata kila timu ikiwa ni idadi kubwa zaidi.

**7-** Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Simba wameruhusu idadi hii ya mabao kwenye nyavu zao na kuwa ndiyo timu iliyofungwa machache zaidi mpaka sasa.

**5-** Namba hii inasimama kwa idadi ya wachezaji waliokosa mikwaju ya penalti kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia michezo 296.

**4-** Inasimama kuwa ni idadi ya mabao yaliyofungwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mjini Arusha, ukiwa ndiyo umeweka rekodi ya kufungwa machache mpaka sasa. Yalipatikana kwenye mechi mbili kati ya African Lyon dhidi ya Yanga na African Lyon dhidi ya Simba. Ikumbukwe kuwa Lyon iliutumia uwanja huo kuwa wake wa nyumbani. Ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Yanga na mabao 3-0 dhidi ya Simba.

**3-** Ni idadi ya 'hat-trick' zilizofungwa mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, zikipigwa na wachezaji Alex Kitenge wa Stand United, Emmanuel Okwi wa Simba na Salum Aiyee wa Mwadui FC.

**1-** Simba ilipoteza mechi pekee dhidi ya Mbao FC, ikichapwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza. Hadi sasa imekuwa ndiyo timu iliyopoteza mechi chache zaidi kwenye ligi hiyo.

**0-** Namba hii inasimama kama tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa ya Lipuli FC. Timu hiyo imefunga mabao 26 na kufungwa 26.

### NAJUA WAJUA

BAO alilofunga Moise Kean wakati Italia ikishinda 2-0 kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Finland juzi, ni la kwanza kwake katika ngazi ya taifa, lakini pia linamfanya kuwa mchezaji kinda wa kwanza kuweza kuifungia timu hiyo tangu Bruno Nicole alipofanya hivyo mwaka 1958, na yosso huyo mwenye umri wa miaka 19, amesisitiza atavunja rekodi zaidi akiwa na 'Azzurri' hao.



## MAKALA




# NYOTA WAKUTOSWA CHELSEA

**LONDON,** England

CHELSEA haijaimarika baada ya kuondoka Antonio Conte. 'Blues' hao bado wanasuasua kwenye Ligi Kuu ya England na wanaonekana watamaliza nje ya nne bora kwenye msimamo. Na wameshaondolewa kwenye mashindano ya ndani kama vile FA na lile la ligi.

Sasa ushindi wa Kombe la Ligi ya Europa ndio unaweza kuwapa matumaini kwa kikosi hicho cha kocha, Maurizio Sarri kuweza kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. Hata hivyo, Sarri anaweza asiwe mtu pekee wa kulaumiwa pale Chelsea. Majina makubwa kama Gonzalo Higuain yameshindwa kufanya lolote kwa Blues hao msimu huu.

Inaeleweka wazi kwamba Chelsea wamepigwa marufuku kufanya usajili, lakini klabu hiyo ina nafasi ya kuwasajili wachezaji wa mkopo ambao wapo tayari kutua hapo. Hivyo, kuwaondoa wachezaji wenye majina makubwa kutaweza kuwapa nafasi wachezaji vijana kutua hapo kwa ajili ya kuimarisha timu.

Hapa tunawaangalia wachezaji watatu ambao Chelsea wanaweza kuwatosa mwishoni wa msimu huu.

**3. Marcos Alonso**

Marcos Alonso bado hajawa na kuwango cha kushawishi kuweza kumpa mkataba mpya. Alijiimarisha kama mmoja wa mabeki bora Ulaya, lakini sasa mambo kwa upande wake hayaendi sawa. Kuboronga kwake kwenye mchezo dhidi ya Everton kulimfanya ashutumiwe zaidi wakati akisababisha penalti dakika ya 72.

Msimu huu unaonekana kabisa kwamba, hayupo kwenye kiwango chake ikilinganishwa na msimu uliopita. Ni wazi kwamba mashabiki wengi wa Chelsea wangependa kumuona Emerson anaanza kwenye kikosi cha kwanza kuliko Alonso.

Emerson raia wa Brazil amejiimarisha mwenyewe kuwa mmoja wa wachezaji wanaoweza kuanza katika kikosi cha kwanza. Huku tayari kukiwa na Ola Aina atakayetua hapo msimu ujao akitokea Torino alikuwa akicheza kwa mkopo.

Ni wazi kwamba, kuondoka kwa Alonso kutatoa nafasi kwa wachezaji wengine vijana kutua hapo kwa mkopo.

**2. Gonzalo Higuain**

Uamuzi wa Chelsea kuziba nafasi ya Alvaro Morata kwa kumchukua Gonzalo Higuain unaonekana kuwa utani wa msimu. Raia huyo wa Argentina amefunga mabao matatu tu katika mechi saba alizoichezea Chelsea msimu huu.

Mashabiki wengi wa Chelsea waliweka matumaini makubwa kwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Napoli baada ya ujio wake hapo katika dimba la Stamford Bridge miezi kadhaa iliyopita. Uwezo wake wa kufumania nyavu akiwa chini ya kocha Maurizio Sarri kwa kipindi cha nyuma, kuliishawishi Chelsea kumsajili. Bahati mbaya ameshindwa kuonyesha kile alichokuwa akitarajiwa.

Hadi sasa amefunga dhidi ya timu dhaifu tu kwenye Ligi Kuu ya England, dhidi ya Fulham na Huddersfield. Tammy Abraham atarudi hapo Stamford Bridge msimu ujao, huku pia wana mchezaji mwingine anayecheza kwa mkopo, Michy Batshuayi. Hivyo wakimrudisha Higuain Juventus linaweza kuwa jambo zuri zaidi kwa miamba hao wa jiji la London.

**1. Pedro Rodriguez**

Pedro amekuwa mfungaji bora wa Chelsea kwenye Ligi Kuu baada ya Eden Hazard msimu huu. Lakini raia huyo wa Hispania, kwa sasa kiwango chake kimeshuka na ni wazi kwamba anapaswa kuondoka. Chelsea msimu huu wamekuwa hawana washambuliaji wazuri, kwa kuwa mabao yake mengi yamekuwa yakitokea kwenye safu ya kiungo, na yeye hajawa msaada tena kwa timu hiyo.

Mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona amefunga mara mbili tu katika mechi 13 alizoichezea msimu huu. Tayari ana umri wa miaka 30, na muda wake wa kukaa hapo Stamford Bridge ni wazi kwamba unaonekana kuelekea ukingoni.

Christian Pulisic atajiunga na timu hiyo msimu ujao, huku Callum Hudson-Odoi bado akiendelea kujiimarisha mwenyewe na kusubiri mechi zaidi za kucheza. Hivyo, litakuwa jambo bora kwa Chelsea kumuachia Pedro aondoke zake.

NDANI YA 18

HARRY Kane ameifungia England mabao 16 chini ya kocha Gareth Southgate - idadi hiyo ikiwa ni mabao 11 zaidi ya mchezaji yeyote katika kikosi hicho.





MSIMU wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa 2018/2019, unaelekea mwisho wakati sasa ikiwa kwenye robo fainali. Mabao yamekuwa muhimu zaidi kwa klabu kuiwezesha kufika kwenye hatua hiyo. Bila mabao hayo klabu hizo zingeondolewa muda mrefu, lakini kwa kutegemea wafungaji mabao mambo yamekuwa tofauti.

**Uk. 16-17**

# SABABU 3 MESSI KUIPA BARCA MATAJI MATATU




**BARCELONA,** Hispania

MARA zote malengo ya Barcelona ni kushinda katika kila mashindano wanayoshiriki kwa kila msimu. Huku 'Blaugrana' bado wakiwa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na Kombe la Mfalme ['Copa Del Rey'] kwa wakati huu, mazungumzo mengi yanaitabiria timu hiyo kutwaa mataji matatu.

Na hiyo imemfanya nyota wao Lionel Messi kubeba majukumu mazito katika mabega yake, na amekuwa nguzo ya mafanikio kwa miamba hao wa Katalunya tangu mwanzoni mwa msimu huu.

Wakati mashabiki wengi wa Barcelona wakiwa na shauku ya kushinda mataji yote matatu, lakini wanafahamu kwamba, kazi hiyo siyo rahisi tu kama kutamka mdomoni. Hata hivyo, mtu pekee anayeweza kuifanya kazi hiyo kuwa rahisi ni Messi.

Alifanya hivyo wakati akiwa chini ya kocha, Pep Guardiola mwaka 2009 na alirudia tena chini ya Luis Enrique mwaka 2015.

Sasa hapa tunaangalia sababu tatu kwa nini nyota huyo wa Argentina anaweza pia kutwaa mataji matatu chini ya kocha, Ernesto Valvarde msimu huu.

**3. Kiwango chake**

Wakati unapofikiri kwamba umeona kila kitu, Messi anakushtua kwa aina nyingine ya kiwango cha kuvutia. Na kiukweli hilo ndilo limekuwa likitokea msimu huu, zaidi na zaidi amekuwa akifanya mambo yasiyotarajiwa.

Nyota huyo wa Argentina kwa sasa hashikiki akiwa mbele ya goli. Messi kwa sasa anaongoza katika orodha ya wafungaji bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na mabao nane kwa jina lake, wakati huo huo pia akiongoza kwenye mbio za kuwania tuzo ya mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Hispania 'Pichichi', akiwa ametikisa nyavu mara 29 na kutoa pasi za mwisho 14 kwenye mechi 26 za La Liga alizocheza msimu huu.

Kwa sasa ndiye mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao mengi katika ligi kubwa tano za Ulaya, na mabao yake mawili katika mechi nne za Kombe la Mfalme yamemfanya kufikisha mabao 39 na kutoa pasi za mwisho 21 kwenye mashindano yote aliyocheza msimu huu.

Nahodha huyo wa Argentina kwa sasa ndiye mchezaji bora zaidi, kwani yupo kwenye kiwango cha juu na anaonekana akiipeleka Barcelona kutwaa mataji matatu msimu huu.

**2. Kikosi kipana**

Baada ya kufanya usajili wenye akili wakati wa soko la kusajili wachezaji, Barcelona sasa ni moja ya timu yenye kikosi imara zaidi barani Ulaya. Wana nyota wakali katika kila idara, na hicho ndiyo kitu kitakachomsaidia Messi kuwaongoza 'Blaugrana' hao kwenye kutwaa mataji matatu.

Tofauti na misimu michache ya nyuma, Barcelona inaonekana kuimarika na kucheza kwa kiwango kizuri zaidi. Nyota wake wana bamba zaidi na wanaonyesha ubora wa hali ya juu, huku wengine wakiwa wanasubiri kule kwenye benchi.

Kwa uwapo wa wachezaji kama Ousmane Dembele, Philippe Coutinho, Arthur Melo na Arturo Vidal, kunamfanya Messi kuwa na kazi rahisi zaidi ya kuisaidia timu yake dimbani.

Kwa muunganiko wa wachezaji hao, Messi anakuwa na kazi rahisi ya kutengeneza pasi za mwisho na kufunga mwenyewe kwa ajili ya kuisaidia timu yake.

**1. Nafasi ya Barca kwenye mashindano yote**

Kushinda mataji matatu kwa msimu mmoja ni jambo gumu zaidi hata kwa timu imara zaidi Ulaya. Hata hivyo, ukiangalia nafasi ya Barcelona kwa sasa, inaonyesha kwamba inaweza kuwa kazi rahisi zaidi kwake.

Miamba hao wa Katalunya wanaongoza kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, kwa tofauti ya pointi 10 dhidi ya Atletico Madrid ambao wanashika nafasi ya pili, na huku zikiwa zimebaki mechi 10 kumalizika kwa ligi hiyo. Wapo kwenye fainali ya Kombe la Mfalme na vijana hao wa Valvarde wamefuzu kwa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambapo wanacheza na Manchester United.

Ukiangalia maendeleo ya Barca kwenye mashindano yote katika hatua hii, inaonyesha wazi kwamba wana nafasi kubwa ya kutwaa mataji matatu msimu huu. Kama Messi ataendelea kuwa kwenye kiwango chake cha sasa, halitakuwa jambo la kushangaza akiibebesha mataji matatu Barcelona msimu huu.

**USILOLIJUA**

CALLUM Hudson-Odoi ni mchezaji kinda zaidi kuweza kuichezea England kwa mara ya kwanza kwenye mechi za kimashindano, akipata fursa hiyo akiwa na umri wa miaka 18 na siku 135.





## Wachimbaji madini kushirikiana na jamii kupunguza migogoro

**Na Mwandishi Wetu,**
CHUNYA

WACHIMBAJI wadogo wa madini katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, wameshauriwa kushirikiana na jamii inayowazunguka ili kuondoa migogoro.

Wito huo ulitolewa na mchimbaji mdogo aliyewekeza kwenye sekta ya madini wilayani humo, Joseph Mwazyele, aliyesema kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara baina ya wachimbaji na wananchi ambayo inakwamisha shughuli za kujiletea maendeleo.

Alisema wachimbaji hao wanapaswa kushirikiana na jamii katika kuchangia shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo sekta ya afya, elimu na miundombinu mingine na kwamba kupitia shughuli hizo watatengeneza uhusiano mzuri.

Alisema wanaitegemea jamii inayowazunguka, hivyo inapotokea suala la migogoro kati yao na wananchi inakwamisha maendeleo ya kiuchumi ya wilaya na taifa, kwa kuwa asilimia kubwa ya watu wanaofanya kazi kwenye migodi inayomilikiwa na wawekezaji wadogo ni wananchi.

"Kuna sababu mbalimbali ambazo zinasababisha migogoro baina ya wawekezaji na wananchi katika maeneo ya uchimbaji madini, moja wapo kugombania mipaka na kufanya shughuli za madini bila ridhaa ya mmiliki," alisema Mwazyele.

Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi MaryPrisca Mahundi, alipiga marufuku wananchi kuvamia mgodi wa mwekezaji huyo na kufanya shughuli za uchimbaji madini na kwamba atayebainika atafikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Maryprisca alisema mwekezaji huyo anafanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria, hivyo ana sifa zote za kuwekeza na kumtaka kushirikiana na jamii inayomzunguka ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa wananchi hao.

# Mbeya yapewa bil. 300/- kuboresha miundombinu

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

SERIKALI imetoa zaidi ya Sh. bilioni 300 mkoani Mbeya kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu, afya, maji, umeme, barabara na shughuli nyingine ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015/20120.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo jana, wakati akihitimisha hafla fupi iliyokuwa imeambatana na matembezi ya amani ya kupongeza na kuunga mkono juhudi za Rais Dk. John Magufuli kwa kutekeleza Ilani ya (CCM).

Chalamila alisema, fedha hizo zimesaidia kukamilisha miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa vituo vya afya na zahanati na kwamba baadhi ya wananchi sasa hawatembei umbali mrefu wala kutumia gharama kubwa kutafuta huduma za afya.

Vile vile ujenzi wa shule za kata umesaidia watoto kutotembea umbali mrefu kwenda shuleni ikilinganishwa na awali wakati changamoto hiyo ilisababisha athari kwa watoto wa kike.

"Katika haya lazima wananchi tumpongeze Rais Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia, nina aimani mkoa wetu anaupenda ndio maana anaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukarabati na kujenga miundombinu mbalimbali ikiwamo barabara," alisema Chalamila.

Chalamila aliwataka watumishi wanaosimamia ujenzi wa miradi kuwa waaminifu ili ijengwe kwa kiwango kinachotakiwa na ikamilike kwa wakati na kwamba atayebainika kutafuna fedha za Rais Magufuli atatafuta mlango wa kutokeo.

"Nitashangaa kuona mtumishi anatafuna fedha za miradi, mnasahau kuwa fedha za Magufuli ni kama maji ya betri ukiyanywa unalo, nawaomba muwe waaminifu mtekeleze miradi kwa wakati ili mlete maendeleo," alisisitiza Chalamila.

Akizungumzia utendaji kazi wa Rais Dk. Magufuli, Mkurugenzi wa Mbeya Vijijini, Steven Katemba, alisema wilaya yake imekuwa ni miongoni mwa wanufaika wakubwa wa fedha za ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.

Alisema Wilaya ya Mbeya ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa vituo vitatu vya afya ikiwamo Santilya ambavyo vimejengwa kisasa na tayari vimekamilika.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi, Wilaya ya Mbeya Mjini, Gervas Ndaki, katika risala yake alieleza kufurahishwa na serikali kulipia gharama za uendeshaji wa shule za msingi na sekondari na kuwasaidia watoto wa maskini kusoma shule.

Alisema elimu bure imepunguza watoto wa mitaani na waliokuwa wanatumikishwa kama mayaya majumbani.

Mwenyekiti wa CCM Mbeya mjini, Afrey Nsomba, alisema wanaMbeya wana imani na Rais Magufuli kuwa bado ataendelea kufanya makubwa ya maendeleo mkoani humo kwa maslahi ya wananchi wote.

Alisema CCM Wilaya ya Mbeya mjini imejipanga kwa ajili ya uchaguzi na kwamba jimbo hilo litarudi mikononi mwa Chama Cha Mapinduzi.



Viongozi mbalimbali wa Chama Cha Mapinduzi na watumishi wa serikali, Wilaya ya Mbeya Mjini akiwamo Mwenyekiti wa CCM Mbeya Mjini, Afrey Nsomba (wa tatu kushoto aliyevaa shati la kijani) na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Wiliam Ntinika (mwenye miwani na kofia), wakiongoza maandamano ya amani ya kumpongeza Rais Dk. John Magufuli kwa kutekeleza Ilani ya Chama kwa kiwango kikubwa. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbarali yajihakikishia 100% vyoo bora

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, imejihakikishia kufikia asilimia 100 ya wananchi wake kuwa na vyoo bora na kwamba ambaye hajatimiza sharti hilo hatua za sheria zitakuchuliwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema kufikia mwezi Machi 30, mwaka huu, kila kaya lazima iwe na choo bora kama walivyotoa maelekezo na hawatakuwa tayari kumsikiliza mwananchi ambaye hajatekeleza agizo hilo, badala yake atakuchuliwa hatua za kisheria.


Alisema mpaka sasa halmashauri hiyo imefikia asilimia 59 ya ujenzi wa vyoo bora na kwamba kwa kushirikiana na wadau wanaendelea kuwahamasisha wananchi kujenga vyoo hivyo, ili kufikia asilimia 100 kama agizo la serikali linavyotaka.

Mfune alidai kuwa suala la ujenzi wa choo bora si la hiari bali ni la kisheria hivyo ni lazima litekelezwe kwa kuwa ni jambo linalohusu afya ya wananchi, hivyo halipaswi kupuuzwa na mtu yeyote.

"Naagiza, hadi kufikia mwezi Machi 30, mwaka huu, kila kaya ihakikishe inakuwa na choo bora ili tuweze kumalizia asilimia 41 hatuna mchezo katika hili lazima litekelezwe," alisema Mfune.

Alisisitiza kuwa Wilaya ya Mbarali haitakuwa tayari kuingia gharama yoyote ya kumhudumia mwananchi atayeugua kipindupindu wakati amekaidi kujenga choo bora.

Aliwaeleza watendaji na wataalamu wa vitongoji, vijiji na kata zote kulisimamia kikamilifu kwa kukagua maeneo ambayo utekelezaji umefanyika na kuhamasisha kwa maeneo ambayo bado hawajaanza ujenzi.



# Viguta kortini tuhuma za utapeli

**Na Augusta Njoji,**
CHAMWINO

BAADHI ya wananchi wa wilayani Chamwino mkoani Dodoma waliioomba kujengewa nyumba za bei nafuu na Muungano wa Vicoba Tanzania (Viguta), wameingiwa na hofu ya usalama wa fedha zao wakidai muungano huo umeingia mitini.

Kufuatia sintofahamu hiyo, Anastazia Lugano, mkazi wa Chamwino, ameushtaki mahakamani muungano huo akidai kurejeshewa Sh. milioni 3.3 alizolipa kwa muungano huo ikiwa ni asilimia 10 ya malipo ili kujengewa nyumba mbili zenye thamani ya Sh. milioni 30.

Akitoa maelezo ya madai yake mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Chamwino, Hamisi Makala, Lugano alidai uongozi wa muungano huo ulifika katika Kijiji cha Chamwino Ikulu Mei, 2017, ukihamasisha wananchi kujengewa nyumba hizo.

Alidai baada ya kuhamasishwa kupitia mkutano wa kijiji uliotishwa na serikali ya kijiji, aliamua kuingia katika mradi huo kwa kulipa Sh. 30,000 za malipo ya fomu na Sh. milioni tatu za malipo ya awali (asilimia 10 ya Sh. milioni 30 ili kujengewa nyumba mbili -- kila moja ikigharimu Sh. milioni 15).

Alidai mahakamani kuwa alipatiwa namba ya akaunti ya muungano huo iliyoko Benki ya NMB na baada ya kulipa, alimkabidhi stakabadhi Hilda Kadunda ambaye kipindi hicho alikuwa Meneja wa Viguta Chamwino.

"Niliwaonyesha kiwanja cha kujenga nyumba hizo mbili, lakini nilianza kuzungushwa hadi sasa nyumba hazijajengwa, nimeamua kuchukua hatua za kisheria ili nipate haki yangu," Lugano alidai.

Meneja wa Viguta Chamwino (Kadunda) aliidai mahakamani kuwa alipokea stakabadhi za malipo ya mlalamikaji huyo akiwa msimamizi wa kampuni na kukiri kuwa viongozi wa muungano huo walimwomba asimamie, lakini amejikuta katika wakati mgumu baada ya kuingia mitini, huku wakisababisha hasara kwa wananchi wa Chamwino.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Makala aliwaagiza madai na mdaiwa wapeleke mashahidi mahakamani. Mashahidi wanaotakiwa ni pamoja na Mwenyekiti na Mtendaji wa Kijiji ili shauri hilo liendelee kusikilizwa na kutolewa uamuzi. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi 26, mwaka huu, yaani kesho.

## Mahitaji ya maji yaongezeka kwa kasi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amesema mahitaji ya maji yanaongezeka kwa kasi kubwa nchini kutokana na ukuaji wa uchumi.

Alitoa kauli hiyo jijini Dodoma mwishoni mwa wiki alipofunga kilele cha Wiki ya Maji.

Alisema mahitaji ya maji katika sekta za uzalishaji mfumo wa umeme, kilimo na viwanda yamekuwa yakiongezeka kwa kasi kadri uchumi unavyokua.

"Pia mahitaji ya maji yanaongezeka kutokana na idadi ya watu. Asilimia 60 ya watu wamefikiwa na huduma ya maji," Prof. Mbarawa alisema.

Alisema kila mwaka wadau hukutana kujadili changamoto za maji na kuzitatua ili wananchi wapate huduma ya uhakiki ya maji.

Alisema lengo ni kuona kila mwananchi anajumuika katika upatikanaji wa maji, huku akiwataka watendaji kuacha kukaa ofisini na kwenda kuona kama wananchi wanafikiwa na huduma ya maji.

Wilhelmina Malima, mwakilishi wa Shirika la Tawasanet, alisema wananchi watarajie mambo makubwa katika uzalishaji wa maji kwa kuwa wamejipanga kushirikiana na serikali kutatua changamoto za sekta hiyo.



Meneja Uendelezaji Biashara Benki ya NMB, makao makao makuu, Masato Wasira, akitoa mada kuhusu huduma zinazotolewa na benki hiyo, ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato ya serikali kwenye mkutano wa wadau wa maji nchini uliofanyika jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri, taasisi 300 rasmi malipo ya kidigitali

**Na Mwandishi wetu,**
DODOMA

BENKI ya NMB imeziunganisha taasisi 300 na halmashauri 180 kwenye mfumo wa ulipaji na ukusanyaji wa mapato serikalini (GePG).

Meneja Uendelezaji Biashara wa benki hiyo Makao Makuu, Masato Wasira, aliyasema hayo alipotoa mada kwenye mkutano wa wadau wa maji nchini uliofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki.

Wasira alisema NMB pia imefanikiwa kuziunganisha mamlaka za maji 22, idara za maji tano na bodi za mabonde ya maji saba katika mfumo huo wa malipo kupitia benki hiyo.

Alisema kupitia mfumo wa GePG, wateja wanaweza kulipia miamala ya ankara za maji kupitia mitandao ya simu za mkononi au matawi ya NMB 220 yaliyoko katika maeneo mbalimbali nchini.

Aliongeza kuwa wateja hao pia wanaweza kulipia ankara zao maji kupitia mawakala wa NMB zaidi ya 6,000, intaneti na kupitia huduma ya NMB Mobile.


Alisema benki hiyo ina wateja zaidi ya milioni 2.5 na imetoa ajira kwa wafanyakazi zaidi ya 3,000 na inapatikana karibu wilaya zote nchini.

Alisema benki hiyo inatoa huduma kwa makundi yote kuanzia kwa wafanyabiashara, wakulima, kampuni, taasisi na serikalini.

Meneja Mwandamizi Uhusiano Serikalini wa NMB Makao Makuu, Amanda Feruzi, alisema benki hiyo ilipata faida ya zaidi ya Sh. bilioni 106 baada ya kodi.

Alisema kupitia ukusanyaji wa mapato ya serikali imeweza kuisaidia serikali kutimiza mipango yake kwa wakati kama ilivyokusudiwa.

Kupitia utoaji huduma bora unaotolewa na NMB nchini, benki hiyo imetajwa na Taasisi ya Kimataifa ya Euromoney kuwa benki bora Tanzania mara sita.



# Shein awataka walimu kuwa wabunifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka walimu nchini kuwa wabunifu na kujiendeleza kitaaluma ili waweze kukidhi mahitaji ya kielimu na kwenda sambamba na wakati.

Dk. Shein aliyasema hayo katika ufunguzi wa Shule ya Msingi ya Fuoni/Pangawe, iliyopo Wilaya ya Magharibi B Unguja.

Alisema ujenzi wa shule hiyo uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni tano ni wa tatu kufanyika, ikiwa ni mwendelezo wa misaada ya serikali ya Jamhuri ya watu wa China kwa Zanzibar, ikitanguliwa na ujenzi wa shule za Kijichi na Urafiki, iliyoko Mwanakwerekwe.

Alisema elimu ni fani inayokuwa na kuendelea siku hadi siku, hivyo ni vyema kwa walimu kwenda sambamba na mabadiliko hayo ili kukidhi haja na kuwa na mbinu mpya za ufundishaji. Dk. Shein alizitaka mamlaka zinazosimamia uendeshaji wa shule hiyo kushirikiana na kuweka walimu wenye uwezo wa kitaaluma, wanaopenda kujituma na wenye kuweka mbele uzalendo ili ufanisi unaotarajiwa uweze kupatikana. “Ni busara tukaiacha ile tabia ya kuwafundisha watoto wetu yale tuliyosoma sisi miaka iliyopita, tuelewe kuwa elimu si sawa na maji ya vidimbwi yanayotuama, bali ni fani inayokuwa na kuendelea siku hadi siku,” alisisitiza Dk. Shein.

Alisema kuwa ufunguzi wa shule hiyo ni uthibitisho wa dhamira njema ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha miundombinu inayochochea maendeleo, ikiwamo ya elimu.

Aidha, alisema ujenzi huo umetokana na mipango ya serikali, iliyozingatia ripoti ya sensa ya watu na mkazi ya mwaka 2012, pamoja na ripoti ya utafiti ya watoto walio nje ya shule. Dk. Shein alisema kuwa ripoti hizo zimeonyesha ongezeko kubwa la idadi ya watu, jambo lililopaswa kwenda na mahitaji ya kijamii, ikiwamo shule na kwamba wilaya hiyo ina jumla ya watoto 36,666 wenye umri wa kati ya miaka sita na 11, ambao ni wajibu kwao kupata elimu ya msingi. “Ripoti hizo zimebainisha kuwapo msongamano mkubwa wa wanafunzi unaofikia wastani wa wanafunzi 90 kwa darasa moja katika shule za wilaya hiyo, ikibainishwa ndiyo zinazoongoza katika changamoto ya aina hiyo,” alisema Dk. Shein. Hata hivyo, alisema uwapo wa shule hiyo utasaidia upatikanaji wa nafasi za masomo kwa watoto wa maeneo hayo na hivyo kupunguza msongamano katika shule za Kinuni, Kijitoupelea, Chunga na Fuoni, ambazo hivi sasa zina wanafunzi 17,054 ikiwa wastani wa wanafunzi 131 kwa darasa moja.

Dk. Shein aliwataka wananchi kudumisha amani pamoja na kuchangamkia fursa za kuendeleza elimu kwa kuwaandikisha watoto wote waliofikia umri wa kuanza shule pamoja na kuwahimiza kushughulikia masomo yao kwa maslahi yao na taifa kwa ujumla.

Alisema mafanikio ya kielimu yaliyofikiwa yanatokana na juhudi na misingi bora iliyowekwa na mwasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume, aliyelenga kuhakikisha vijana wote wanapata elimu bila ubaguzi.

Naye, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pemba Juma, alisema ujenzi wa shule hiyo ni moja kati ya tatu zilizotangulia kujengwa, ukiwa umevuka malengo ya Ilani ya CCM 2015 - 2020.

Alisema kupitia ugatuzi wizara hiyo itashirikiana na Wizara ya Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika usimamizi wa suala zima la ufundishaji.



Ofisa wa Dawati la Jinsia la Magereza mkoani Shinyanga, Victoria Kizito, akichangia mada kwenye mkutano wa wadau wa kupinga masuala ya ukatili wa kijinsia, ulioandaliwa na Shirika la Agape, Cuso na TGNP na kutaka elimu hiyo ya ukatili pia ikatolewe kwa wafungwa hasa wa kiume ambao wanadaiwa kufanya ngono kinyume na maumbile. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Cuba kuendeleza ushirikiano wa kidiplomasia na Tanzania

**Na Waandishi Wetu**

CUBA itaendelea kudumisha ushirikiano wa kidiplomasia na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mafungamano ya kustawisha wananchi wake licha ya taifa hilo la Caribean kipindi hiki kupita katika mabadiliko ya kisiasa, uchumi na utamaduni.

Rais wa Bunge la Cuba, Esteban Lazo Harnandez, aliyasema hayo wakati wa mazungumzo na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Iddi, aliyefika kusalimiana naye na kumpongeza baada ya kuchaguliwa tena kuliongoza Bunge hilo katika Ofisi za Bunge Mjini Havana, nchini Cuba.

Lazo Harnandez, alisema kutokana na mabadiliko ya mfumo wa dunia uliopo hivi sasa katika masuala ya uchumi, siasa na utamaduni, Jamhuri ya Cuba imelazimika kufanya mabadiliko ya Katiba yake ili yalingane na mfumo huo wa dunia inayozunguka katika mazingira ya kijiji.

Alisema Bunge la Cuba tayari limeshafanya marekebisho katika Katiba yake kutoa nafasi kwa wananchi wake kuwa na uwezo na uhuru wa kumiliki nyumba, ardhi pamoja na uwepo wa Waziri Mkuu atakayekuwa na mamlaka ya kusimamia utendaji wa serikali.

Alimweleza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwamba wakati vikao vya Bunge hilo vinavyotarajiwa kuanza wiki ijayo baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa wabunge wake, serikali ya nchi hiyo imeanza kupiga hatua kubwa zaidi ya maendeleo kutokana na mabadiliko hayo.

Rais huyo wa Bunge la Cuba, alisema kwamba taasisi za kifedha zitalazimika kuzingatia ukusanyaji bora zaidi wa mapato katika maeneo yote ya uchumi ili ushiriki wa wananchi waliowengi katika mfumo huo wa kifedha upatikane vyema.

Esteban alimhakikishia Balozi Seif kwamba uhusiano wa muda mrefu uliopo kati ya pande hizo mbili utaendelea kuimarishwa na kukuzwa katika muda wote.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Iddi, alisema Zanzibar na Tanzania kwa ujumla zitaendelea kufuatilia mabadiliko ya Cuba na kuangalia hatua inayoweza kuiga mabadiliko hayo katika azima ya kuimarisha uchumi na ustawi wa wananchi walio wengi.

Balozi Iddi katika mazungumzo hayo alimpongeza Rais wa Bunge hilo la Cuba kwa kuchaguliwa tena kushika wadhifa huo ikionyesha wazi ishara halisi ya kukubalika vyema na wananchi wa nchi hiyo kupitia viongozi wake.

Balozi Iddi na ujumbe wake alimalizia ziara yake nchini Cuba kwa kufanya mazungumzo na uongozi wa Waziri wa Afya wa nchi hiyo ukiongozwa na Naibu Waziri wake, Marcia Cobas hapo Makao Makuu ya Wizara ya Afya mjini Havana.

Katika mazungumzo yao ya ushirikiano wa kindugu Balozi Seif alisema matunda ya Darasa la Madaktari Wazalendo waliosimamiwa na wataalamu pamoja na wahadhiri wa nchi ya Cuba, yameanza kutoa matumaini.

Balozi Iddi alisema kitendo cha Serikali ya Cuba kukubali kupunguza gharama kubwa ya kuwaendeleza madaktari hao wazalendo wapatao 15 katika shahada ya juu ya udaktari wa uzamili nchini humo, kinaendelea kuleta faraja kubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na watu wake.

# Serikali kufuatilia hali ya afya ya wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa Serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi umesema utaendelea kuwasaidia na kufuatilia kwa karibu hali ya afya ya wananchi wake ambao wamekuwa wakisumbuliwa na maradhi mbalimbali ili kuona zinazidi kuimarika na wanarejea katika shughuli zao kama kawaida.

Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, alieleza hayo wakati wa ziara yake katika Shehia ya Hawaii, Jang’ombe Urusi na Kwalaamsha ya kuwajulia hali na kuwafariji baadhi ya wagonjwa wa mkoa wake.

Alisema serikali ya mkoa huo inathamini mchango mkubwa uliotolewa na wananchi hao katika sekta tofauti kwa Mkoa wa Mjini Magharibi na taifa kwa ujumla, hivyo uongozi wa mkoa utahakikisha unatoa kila aina ya msaada wa hali na mali ili kuona wanapona kwa haraka na kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Aidha, Ayoub aliahidi familia ya aliyekuwa Sheha wa Shehia ya Jang’ombe Urusi, Khamis Ali Khamis, kumpatia baadhi ya huduma ikiwamo bima ya afya kwa kazi kubwa aliyoifanya wakati alipokuwa akitumikia shehia hiyo kwa kipindi kirefu, hata hivyo, Mkuu wa Mkoa aliithibitishia familia hiyo kuwa, ofisi yake itaendelea kuwa karibu muda wote.

Kwa upande wao wanafamilia na wagonjwa hao walielezea furaja na matumaini yao waliyoyapata kwa ziara ya kutembelewa na kiongozi hatua ambayo imewajengea matumaini na imani kubwa kwa uongozi wa mkoa na serikali ya kwenda kuwafariji na kuwajulia hali pamoja na misaada na ahadi mbalimbali alizotoa.

## HABARI KIMATAIFA

## 11 wafariki dunia, Al Shabab wakitekeleza shambulio

**MOGADISHU, Somalia**

SHAMBULIZI la Al Shabab dhidi ya jengo la serikali mjini Mogadishu jana, limegharimu maisha ya watu 11 akiwamo Naibu Waziri wa Kazi, Saqar Ibrahim Abdalla.

Taarifa iliyotolewa na serikali nchini Somalia ilieleza kuwa shambulizi hilo lililothibitishwa kutekelezwa na wanamgambo wa Al Shabab, linaashiria kuwa kundi hilo lenye msimamao mkali bado linauwezo wa kuyumbisha usalama wa nchi.

Seneta, Ilyas Ali Hassan, alithibitisha kwamba Naibu Waziri Abdalla alifariki dunia katika shambulio hilo.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa milipuko miwili iliyotekelezwa katika lango kuu la kuingia ofisi za wizarani ndio ilianza kusikika kabla ya washambuliaji kuvamia majengo ya wizara ya kazi.

Wanawake watatu ni miongoni mwa waliouawa katika shambulizi hilo, ambapo majeruhi ni 15.

Kwa mujibu wa taarifa za Jeshi la Polisi wapiganaji wanne wa Al Shabab walivamia ofisi hizo za serikali kabla ya kusikika kelele za makabiliano na wafanyakazi waliokuwamo katika majengo hayo.

*RFI*

## Wapelekwa jela kwa kuharibu picha ya Rais

**BUJUMBURA, Burundi**

WASICHANA watatu nchini Burundi, wamepelekwa jela wakisubiri kuhukumiwa baada ya kuharibu picha ya Rais wa Burundi, Pierre Nkurunziza, kwenye vitabu vya kusoma.

Imeelezwa kuwa wasichana hao wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 17 iwapo watapatikana na kosa la kumdhihaki Rais, watafungwa kifungo cha miaka mitano.

Majaji wamesema kuwa wasichana hao ni lazima wafunguliwe mashtaka kwa kosa hilo, na kuagiza wazuiwe kwenye jela ya watoto mjini Ngozi Kaskazini mwa nchi hiyo.

Muungano wa mashirika ya kiraia 48 (FENADEB), yamelaani hatua hiyo na kusema haikubaliki na ni ukiukwaji wa haki za watoto.

Wasichana hao wamekuwa wakizuiwa tangu Machi 12, mwaka huu, baada ya kukamatwa pamoja na mvulana mwenye umri wa miaka 13 ambaye baadaye aliachiliwa huru.

Mwanaharakati kutoka Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki za Binadamu, Lewis Mudge, alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali ndio inayoshughulikia kesi hiyo na haijafahamika ni lini kesi hiyo itaanza kusikilizwa.

*RFI*

# Mawaziri Uingereza wapanga kumng'oa waziri mkuu

**LONDON, Uingereza**

VYOMBO vya habari nchini Uingereza vimeripoti kuwa Baraza la Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Theresa May, limekataa kuunga mkono uongozi wake na limemtaka aachie madaraka.

Siku ya Jumamosi usiku, vyombo vya habari nchini Uingereza viliripoti kuwa May alikuwa anakabiliwa na pingamizi kubwa ndani ya baraza lake la mawaziri na huenda akajiuzulu.

Hatua hiyo inakuja siku chache kabla ya kupigwa kura ya tatu kuhusu makubaliano ya May kutaka Uingereza kujiondoa katika Umoja wa Ulaya (EU). Hadi sasa maombi hayo yameshakataliwa mara mbili.

Magazeti ya The Sunday Times, The Telegraph na The Daily Mail yaliripoti kuwa kuna uwezekano wa kutokea kwa mapinduzi, yakiwanukuu wabunge wa chama cha Conservative.

Magazeti hayo pia yaliripoti kuwa kiongozi wa muda atachaguliwa kusimamia wiki za mwisho za mchakato wa kujitoa katika EU.

Gazeti la The Daily Mail liliripoti kuwa waziri wa Mazingira, Michael Gove, huenda akachukua uongozi wa mpito kabla ya kinyang'anyiro kamili kufika.

Mhariri wa siasa wa gazeti la The Times, Tim Shipman, alisema mawaziri wamemgeuka May kwa namna ya kushangaza na wanamshinikiza kuachia madaraka. Aliongeza kuwa mume wa May alikuwa mojawapo ya watu wachache wanaomhimiza aendelee kuwapo kama waziri mkuu.

Mbunge anayeunga mkono Uingereza kujitoa EU, Anne-Marie Trevelyan aliliambia gazeti la The Telegraph kwamba mawaziri wanapaswa kumpa nafasi May.

Mtandao wa habari wa Buzzfeed nchini Uingereza ulieleza kuwa mnadhimu wa serikali, Paul Maynard, alimweleza May kuwa mkakati wake unakiharibu chama chao.

Juzi, zaidi ya watu milioni moja waliandamana katika mitaa ya Jiji la London nchini Uingereza kudai kura ya pili ya maoni.

Waandamanaji hao walikuwa wamebeba mabango yaliyokuwa na ujumbe kwa serikali ukisema "kuondoa kifungu cha 50 na tunaandamana kutaka kura ya watu na pia tunaupenda Umoja wa Ulaya."

Maandamano hayo yalihudhuriwa na watu kutoka vyama vyote ambapo Naibu Kiongozi wa chama cha Labour, Tom Watson, alisema anaunga mkono kura ya pili ya maoni kama njia pekee ya kutatua mkwamo wa Uingereza kujitoa EU.

Pia waziri kiongozi wa Scotland, Nicola Sturgeon na kiongozi wa chama cha Liberal Democrats, Vince Cable, walishiriki maandamano hayo.

*DW*



Mwanajeshi wa Somalia akiokoa majeruhi katika jengo lililoshambuliwa mjini Mogadishu. **PICHA: REUTERS**

# Idadi waliofariki kwa kimbunga yafikia 615

**HARARE, Zimbabwe**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Uratibu wa Misaada ya Kibinadamu (OCHA), limesema idadi ya watu waliofariki kwa kimbunga Idai katika nchi za Msumbiji, Zimbabwe na Malawi imefikia 615.

Limesema nchini Msumbiji watu waliofariki ni 417, Zimbabwe 139 na Malawi 59.

Zimbabwe imeshapeleka maombi Jumuiya ya Kimataifa ipatiwe msaada wa dawa, chakula na ujenzi wa miundombinu.

"Tangu kimbunga Idai kupiga eneo hilo, tunahangaika kupata chakula, nguo zetu zilichukuliwa na maji, na hivi sasa hatujui cha kufanya," alisema Indalo mmoja wa waathirika wa kimbunga hicho.

Alisema serikali iliahidi kuwasaidia kwa kuwapa hifadhi ya mahali pakuishi, lakini inaelekea kuwa msaada huo utakwenda hata kwa watu ambao hawakuathiriwa na mafuriko.

"Nimempoteza baba yangu, na bado tunamtafuta ndugu yangu. Inauma sana. Hatuna chakula wala makazi," alisema.

Hali hiyo pia inaikabili familia ya Dube-Magoso iliyoko mita 500 kutoka eneo hilo, ambapo baba yao mwenye umri wa miaka 83 alikufa wakati nyumba yao ilipobomoka na kimbunga hicho, huku mama yao akinusurika.

Mtoto wao, Musavengana Dube Magoso, anasema wanataka serikali ya Zimbabwe kuwasaidia.

"Serikali lazima itutafutie sehemu bora ya kwenda kuishi ili tuweze kufanya kazi na kupata kipato chetu ili sote tuweze kupata njia ya kuendesha maisha yetu," alisema na kuongeza;

"Hadi hivi sasa, hatuna chakula kile tulichokuwa tumepanda, kimeharibiwa na maji. Tumerudishwa nyuma kabisa kimaisha," alisema.

Wafanyakazi wanaosaidia kuokoa maisha ya watu walioathirika na janga hilo, wanasema kuwa mafuriko hayo yaliyofuatia kimbunga Idai ni kama janga kubwa kuliko yote yaliyowahi kutokea katika kipindi cha miaka 20.

Vyanzo vya habari nchini Zimbabwe vimeripoti kuwa bado zoezi la kutafuta wananchi waliopotea linaendelea na huenda taarifa kutoka kwenye maeneo yaliyokumbwa na kimbunga hicho kibaya kilichosababisha mafuriko zikaongeza.

Umoja wa Mataifa (UN) tayari umeongeza kiwango cha msaada wa dharura na limeonya kuhusu uwezekano wa milipuko ya magonjwa.

Nchi hizo tatu za Kusini Mashariki mwa Afrika tayari ziko katika uangalizi wa UN.

*VOA*

# 'Acheni kuwakaririsha wanafunzi masomo'

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

WALIMU wametakiwa kuwafundisha wanafunzi masomo kwa vitendo, ili kuwawezesha kuwa wabunifu na kujua kitu kiuhalisia zaidi.

Hayo yalisemwa na Benjamin Oganga ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Sekondari katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) katika mahafali ya kidato cha sita ya Shule ya Sekondari St. Mathew's, iliyopo Mkuranga mkoani Pwani.

Oganga alisema hayo katika mahafali ya 14 ya shule hiyo, kuwafundisha watoto kwa vitendo kunawasaidia kuwa wabunifu.

"Kuna baadhi ya walimu wamekuwa wakiwafundisha wanafunzi masomo kwa kuwakaririsha hali inayochangia mtoto kutokuwa mbunifu," alisema.

Aliipongeza Shule ya St .Mathew' s kwa kuliangalia hilo la kuwafundisha wanafunzi kwa vitendo ili baadaye waweze kujitambua katika kufanya jambo.

Alisema alipotembelea maonyesho ya vijana wanaohitimu kidato cha sita katika masomo yao, aligundua wanafunzi wamejifunza kwa vitendo kutokana na maneno waliyokuwa wakiyaeleza ikiwamo na vifaa walivyokuwa wakivitumia katika maonyesho hayo na kuvielezea matumizi yake.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Christopher Segereti, shule yao inafundisha masomo kwa nadharia na vitendo, lengo likiwa ni kumwezesha mtoto kujitambua. Aliongeza kuwa shule yao inatambua umuhimu wa kuwafundisha masomo wanafunzi kwa vitendo ili masomo hayo yawe mkombozi kwao hapo baadaye.

"Tunajua ukitaka mtoto ajitambue, inatakiwa umfundishe kwa vitendo na sio kumkaririsha," alisema.

Kwa mujibu wa Segereti, wanafunzi zaidi ya 100, mwezi Mei, mwaka huu, wanatarajia kufanya mitihani ya kidato cha sita.



Vijana kutoka mikoa ya Dodoma, Singida, Morogoro na Pwani wakisikiliza hotuba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Wajasiriamali Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine (SUGECO), Revocatus Kimario, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kilimo biashara na ujasiriamali yaliyofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo katika kambi ya vijana ya kilimo na maarifa mkongo, Wilaya ya Rufiji.

## Mbaroni kwa kukutwa na misokoto ya bangi

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

POLISI mkoani Singida inawashikilia Ally Ramadhani (36), Juma Omari (48) na Hashimu Ramadhani (19), wilayani Manyoni kwa tuhuma za kukutwa wakiwa na misokoto 147 na gramu 40 za bangi.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida, ACP Sweetbert Njewike, alisema katika tukio la Machi 16, mwaka huu, saa nane mchana, wakati askari wakiwa katika operesheni za kupambana na dawa za kulevya, walikamata wakazi wawili wa mtaa wa Msufini wakiwa na misokoto ya bangi 147.

Aliwataja waliokamatwa kwa tuhuma za kukutwa na misokoto ya bangi kuwa ni Ramadhani (36) na Omari (48), Manispaa ya Singida.

"Mbinu iliyotumika kuificha bangi hiyo chumbani na wamekutwa wakiifunga tayari kwa kuiuza kwa lengo la kujipatia kipato kwa njia isiyo halali," Kamanda Njewike, alisema.

Katika tukio lingine, Kamanda Njewike alisema, jeshi hilo linamshikilia mkazi wa Kijiji cha Mlowa Ziginali, Kata ya Majengo, wilayani Manyoni baada ya askari kumkuta Ramadhani (19), akiwa na gramu 40 za bangi.

Alisema mbinu iliyotumika ni mtuhumiwa kuficha bangi katika mfuko mdogo wa nailoni ili wauze kidogo kidogo kwa lengo la kujipatia fedha isivyo halali.

Kufuatia tukio hilo Jeshi la Polisi linawashikilia watuhumiwa kwa mahojiano zaidi ili kujua mitandao mbalimbali inayojihusisha na biashara ya dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na biashara zingine haramu kwa lengo la kutokomeza vitendo hivyo na wanatarajiwa kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

**"Mbinu iliyotumika kuificha bangi hiyo chumbani na wamekutwa wakiifunga tayari kwa kuiuza kwa lengo la kujipatia kipato kwa njia isiyo halali," Kamanda Njewike, alisema.**

# Uhamiaji yatoa elimu kwa wananchi wa mipakani

**Na Anthony Gervas, MARA**

IDARA ya Uhamiaji imetoa elimu kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka mipaka ya Sirari nchini Tanzania na Isibania nchini Kenya, kuhusu ushirikishwaji wa ulinzi na usimamizi wa mipaka utakaosaidia kuwabaini wahamiaji haramu wanaoingia nchini bila kibali cha kuishi.

Msemaji Mkuu wa Idara ya Uhamiaji, Ally Mtanda, alisema hayo mwishoni mwa wiki katika warsha ya siku tatu iliyofanyika Sirari.

Alisema ushirikishwaji huo wa wananchi wa nchi zote mbili utasaidia katika utambuzi wa kuwafichua wahamiaji hao na watu wanaowaficha majumbani mwao.

"Idara ya Uhamiaji Tanzania imeona kuna haja ya kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya mipakani ya Sirari Tanzania na Isibania nchini Kenya kuhusu ushirikishwaji wa ulinzi na usimamizi wa mipaka, ili waweze kuwa na utambuzi wa kuwabaini wahamiaji haramu na kuwatia mbaroni wanaoingia nchini bila vibali vya kuishi kinyume cha sheria za nchi, alisema Mtanda.

Alisema kuwa hatua hiyo itasaidia kukamata watu wanaojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu kwenda nchi za nje, wahalifu, pamoja na wale wanaojihusisha na biashara za magendo kwa kutumia bodaboda kupitia njia za panya.

Alisema washiriki wa warsha hiyo ni maofisa wa idara mbalimbali za serikali kutoka nchini Kenya na Tanzania wakiwamo maofisa wa idara za afya, mifugo, misitu, watendaji wa vijiji, kata, tarafa, madiwani, polisi, TRA, viongozi wa dini pamoja na siasa. Aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuwa wazalendo wa nchi zao kwa kutoa taarifa kwenye mamlaka husika wanapoona kuna watu wa aina hiyo na kwamba kila mmoja awe mlinzi na msimamizi wa mipaka ili kukomesha tatizo hilo.

Hata hivyo, madereva wa bodaboda katika mipaka hiyo ya Tanzania na Kenya wanatajwa kuwa wanaoongoza kwa kuvusha mizigo ya biashara haramu za magendo kwa kutumia njia za panya, badala ya kupita kwenye njia halali, kwa lengo la kukwepa kulipa kodi ama ushuru.

Aidha, Meneja wa Kituo cha Forodha cha Sirari mkoani Mara (TRA), Martin Kawonga, aliwaonya madereva bodaboda wanaojihusisha na biashara haramu za kuvusha mizigo ya magendo kwa njia za panya kuacha mara moja na watakaokamatwa watafikishwa katika vyombo vya dola ikiwamo kutaifishwa mali zao na bodaboda zao.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja vinauzwa chanika mita 100 kutoka stendi mpya ya Chanika umeme upo bei kuanzia 2m vimebaki vichache. Mawasiliano: 0714-187555 au 0755-288879

### NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI UALIMU / CERTIFICATE** au diploma / english/mathematics na science 0656490706/0655628640


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### CHETI KIMEPOTEA



115135902

**ALPHONCE LUKANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0385/0131** kilichotolewa na Shule ya Sekondari Ujiji – Kigoma mwaka 2008. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KGM/RB/803/2019.**

### KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI

**BENEDICT MICHAEL MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 648 BQH** TOYOTA PRADO. Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 680 CAP TOYOTA** CARINA. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/B/I/VOLXX/240.**

115136102


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 46/2017.**

**Ombi la RAHIMU HUSSEN kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu HUSSEN SALEHE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 12/4/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.



115135702


**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

au piga simu: 0767 223 311

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO,
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# VARANE AKANA UVUMI MADRID

**MADRID, Hispania**

BEKI wa Real Madrid, Raphael Varane, amekanusha taarifa kwamba hana furaha kucheza katika klabu hiyo ya Hispania, huku uvumi ukienea kwamba majaliwa yake hapo kwenye dimba la Santiago Bernabeu yapo shakani.

Taarifa za hivi karibuni zinasema kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anataka kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto ili kwenda kutafuta changamoto mpya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye kwa sasa yupo na Timu ya Taifa ya Ufaransa, amebainisha kwamba sio kweli kuwa hana furaha hapo Real Madrid.

Akinukuliwa na Gazeti la Metro, Varane alisema: "Kusema kwamba sina furaha pale Real Madrid si kweli.

"Mimi nipo Real Madrid. Klabu kubwa zaidi duniani. Kwa sasa nina changamoto yangu binafsi, lakini ukweli ni kwamba nina furaha kuichezea Real Madrid.

"Tulikuwa na mwanzo mgumu wa msimu, lakini tunapigana kuhakikisha tunarudi kwenye nafasi yetu."




# MAN UNITED
## BAYERN KWA HUDSON-ODOI

**LONDON, England**

KLABU ya Manchester United inapanga kuingia kwenye mbio moja na Bayern Munich kuwania kumsajili winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi.

Bayern Munich imeonyesha nia thabiti ya kutaka kumsajili mchezaji huyo, ikiwa tayari ilishatoa ofa ya pauni milioni 35 Januari, lakini walishindwa kukamilisha dili hilo na 'Blues' hao.

Liverpool na Borussia Dortmund pia zimetajwa kuwania saini ya mchezaji huyo kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail, lakini sasa United inajiandaa kutuma ofa zaidi kwa Hudson-Odoi, huku taarifa nyingine zikieleza kwamba mchezaji huyo anakaribia kusaini mkataba mpya hapo Stamford Bridge.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2020, hivyo Chelsea wanaweza kuwa kwenye hatari ya kumkosa mchezaji huyo wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Hakuna mazungumzo yoyote ambayo yamefanyika hadi sasa tangu Januari kuhusu kuongeza mkataba wake mpya, hivyo Chelsea inatakiwa kufanyia kazi haraka.

Mshambuliaji huyo bado hajaanza kucheza kwenye mchezo wowote wa Ligi Kuu chini ya kocha, Maurizio Sarri.

Hudson-Odoi alipewa nafasi ya kuichezea kwa mara ya kwanza Timu ya Taifa ya England wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Jamhuri ya Czech mwishoni mwa wiki.

# Fernandes atengewa fungu kubwa United

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inatarajia kutenga kiasi cha pauni milioni 250 kwa ajili ya kuwasajili nyota wa Ureno, Joao Felix, Ruben Dias na Bruno Fernandes.

Kocha wa muda wa timu hiyo, Ole Gunnar Solskjaer anapanga kukiimarisha kikosi hicho, huku kukiwa na uwezekano wa kupewa mkataba wa kudumu kuifundisha klabu hiyo wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa United ameonyesha nia ya kutaka kuwasajili wachezaji hao kwa ajili ya kukijenga zaidi kikosi chao kwa msimu ujao, kwa mujibu wa Gazeti la Mirror. Na kocha huyo katika orodha yake amewaweka wachezaji hao wa Benfica, Felix na Dias pamoja na nyota wa Sporting CP, Fernandes.

Hata hivyo, bei ya wachezaji hao kwa pamoja inatajwa kuwa ni pauni milioni 250, huku Felix mwenye umri wa miaka 19, akitajwa kuwa pauni milioni 105, huku Dias mwenye umri wa miaka 21 gharama yake ikitajwa kuwa ni pauni milioni 50 na Fernandes mwenye umri wa miaka 24 anatajwa kuigharimu United pauni milioni 95.

United sio klabu pekee inayowawania wachezaji hao, kwani pia miamba wa Ulaya, Barcelona, Real Madrid, Juventus na Manchester City pia zinatajwa.



## HABARI MICHEZO



# POGBA

## AFUNGUKA KINACHOMVUTIA BARCA

Pogba

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, amesema kwamba, huwa anavutiwa zaidi kuitazama Barcelona ikiwa inacheza.

Kauli ya Pogba inakuja wakati Man United ikijiandaa kuivaa Barcelona kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pogba anatarajiwa kuwa sehemu ya kikosi kitakachocheza dhidi ya wababe hao wa Hispania mwezi ujao, lakini amesema amekuwa akivutiwa kuitazama Barcelona mara nyingi.

"Barcelona ni timu ambayo mara nyingi naitazama, unaweza kujifunza kama kiungo, wanacheza soka zuri, tamaduni yao na mengine mengi yanaweza kunifunza," alisema akinukuliwa na Sky Sports.

"Barcelona ni moja ya timu bora duniani, wana wachezaji wengi wazuri, mechi dhidi yao naamini itakuwa nzuri.

Nilicheza nao katika fainali ya Ligi ya Mabingwa mwaka 2015 nikiwa Juventus," alisema Pogba.

Kiungo huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 26, amekuwa akihusishwa kuwaniwa na timu kubwa za Ulaya.

Mbali na hapo amepongeza muundo wa Barcelona na kueleza kuwa staa wa timu hiyo, Lionel Messi bado ni mchezaji mwenye kiwango cha juu.

"Messi ni mchezaji bora wa muda wote, Barca ina wachezaji wengi wazuri," alisema Pogba.

# Mbappe aongoza kura kutakiwa Real Madrid

**MADRID, Hispania**

MASHABIKI wa Real Madrid wameamua kwenda mitandaoni kupiga kura za kuitaka klabu yao kuwanunua baadhi ya mastaa nyota katika dirisha kubwa lijalo la uhamisho.

Majina ya Kylian Mbappe wa PSG, Paul Pogba wa Manchester United, Matthijs de Ligt wa Ajax na Eden Hazard wa Chelsea yameonekana kupigiwa chapuo katika kura za mashabiki wa Real Madrid zilizoendeshwa na gazeti maarufu la michezo nchini Hispania, Marca.

Zaidi ya mashabiki 200,000 walipiga kura hizo na jina la Mbappe lilionekana kuteka hisia za mashabiki wa timu hiyo maarufu zaidi duniani, ambako asilimia 79 ya kura zilikwenda kwa Mbappe mbele ya nyota wengine kama staa mwenzake wa PSG, Neymar pamoja na staa wa Tottenham, Harry Kane.

Mashabiki hao waliambiwa wachague wachezaji wanaowataka katika nafasi tofauti ambako katika nafasi ya ulinzi waliwekewa majina kama ya mlinzi wa Ajax, Matthjis De Ligt, mlinzi wa Inter Milan, Milan Skriniar, na mlinzi wa Napoli, Kalidou Koulibaly ambaye jina lake limekuwa likihusishwa zaidi na Manchester United.

Katika kura za eneo la ulinzi, De Ligt ambaye ni nahodha wa Ajax akiwa na umri wa miaka 19 tu aliwakimbiza wenzake na kupata asilimia 67 ya kura zote. Hata hivyo, kinda huyo amekuwa akihusishwa zaidi kwenda kwa wapinzani wa Real, Barcelona alikotangulia nyota mwenzake Frenkie De Jong.

Kwa upande wa walinzi wa pembeni, Chelsea inabidi ikae mkao wa kuvamiwa baada ya jina la mlinzi wao wa kushoto, Marcos Alonso, kupata kura nyingi mbele ya mlinzi wa kushoto wa Bayern Munich, David Alaba, ambaye awali ilidhaniwa angeweza kuibuka mshindi.

Katika eneo la kiungo, staa wa Manchester United, Paul Pogba, ambaye katika siku za karibuni alikaririwa na vyombo vya habari akidai kwamba Real Madrid ni timu ya ndoto zake, alionekana kuwaburuza wenzake katika eneo hilo.

Jina lake lilipata kura nyingi mbele ya mastaa wenzake kama vile kiungo wa Lazio na timu ya Taifa ya Serbia, Sergej Milinkovic-Savic, nyota wa Bayern Munich, Thiago Alcantara, na kiungo mahiri wa Juventus Turin, Miralem Pjanic.


Kwa upande wa mawinga, staa wa Chelsea, Eden Hazard, ambaye ameonekana kuhusishwa zaidi kwenda Real Madrid katika dirisha kubwa la majira ya joto, alipata kura zaidi ya asilimia 70 na kumpita staa wa Tottenham, Christian Eriksen, ambaye pia amekuwa akihusishwa kwenda klabuni hapo.




Katika majina yote haya, mashabiki wamesisimka zaidi na Mbappe ambaye miaka michache iliyopita alikuwa kinda zaidi katika klabu ya Monaco, huku tayari baadhi ya washambuliaji waliowekwa katika orodha yake kina Kane, Neymar, Mauro Icardi na Pierre-Emerick Aubameyang wakiwa majina makubwa.

Mbappe pia amekuwa akihusishwa kwenda Real Madrid ambako kama dili lake likitimia basi atavunja rekodi ya uhamisho ya dunia ambayo iliwekwa na Neymar katika dirisha kubwa la uhamisho mwaka 2017.

# Depay aing'arisha Uholanzi



**AMSTERDAM, Uholanzi**

MEMPHIS Depay akiwa ndani ya jezi ya Uholanzi, ameonyesha kiwango bora na kufanikiwa kufunga mabao mawili katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Belarus.


Timu hizo zilikutana katika mchezo wa makundi kuwania kufuzu kushiriki michuano ya Euro 2020, matokeo ambayo yamemfanya Kocha wa Uholanzi, Ronald Koeman, kuwa na mwanzo mzuri katika mchakato huo ulioanza juzi usiku.

Depay ambaye ni staa wa zamani wa Manchester United, alifunga mabao hayo katika kila kipindi huku mengine yakifungwa na Georginio Wijnaldum na Virgil van Dijk. Ushindi huo wa Kundi C umeifanya Uholanzi kuongoza kundi hilo kabla ya mchezo mwingine wa Ujerumani.

Kwa mabao hayo sasa Depay ambaye alikuwa Mchezaji Bora wa Mechi, amefikisha mabao 10 katika mechi 14 za kimataifa alizoichezea timu yake ya taifa. Mchezo mwingine wa Kundi C, Ireland ya Kaskazini nayo ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Estonia, michezo yote ikichezwa usiku wa juzi.

Katika Kundi E, Croatia ilishinda 2-1 dhidi ya Azerbaijan, Slovakia ikaifunga Hungary mabao 2-0. Kundi G, Austria ikiwa nyumbani ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Poland, Macedonia ya Kaskazini ikashinda mabao 3-1 dhidi ya Latvia, Israel na Slovenia zikatoka sare ya bao 1-1. Kundi I, Kazakhstan 3-0 Scotland, Cyprus 5-0 San Marino, Ubelgiji 3-1 Urusi.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RAMOS AKUNWA NA FALSAFA ZA ENRIQUE

●●● Mara zote unakuwa na ndoto na malengo ya kupata mafanikio fulani muhimu, tupo katika nguvu mpya ya kufanya kazi na mwenye...

**VALENCIA, Hispania**

NAHODHA wa Hispania, Sergio Ramos, amepongeza falsafa za kocha mpya wa Hispania, Luis Enrique, baada ya kushinda mechi yao ya kwanza ya kuwania kufuzu fainali za Euro 2020 juzi, Jumamosi.

Hispania iliichapa Norway kwa mabao 2-1 katika mechi hiyo iliyopigwa Valencia, lakini ilihitaji bao la penalti kutoka kwa Ramos kuweza kubeba pointi zote tatu baada ya Josh King kusawazisha bao la kwanza la Rodrigo Moreno.

Nahodha Ramos sasa amecheka na nyavu katika mechi tano mfululizo alizoichezea Hispania na anadhani timu hiyo kwa sasa ipo katika mikono mizuri baada ya kuteuliwa kocha wa zamani wa Barcelona, Luis Enrique kuinoa. "Mara zote unakuwa na ndoto na malengo ya kupata mafanikio fulani muhimu," Ramos aliiambia TVE.

"Tupo katika nguvu mpya ya kufanya kazi na mwenye falsafa za uchezaji wa kushangaza, kisha tutaona mechi baada ya mechi. Kushinda kutatufanya kujisikia kujiamini zaidi.

"Njia mpya imeanza na kilicho bora ni kuanza kushinda dhidi ya mpinzani ambaye amefanya mambo kuwa magumu licha ya ukweli kwamba tulikaa na mpira? Tulijua kwamba itaumiza."

Kwa upande wake, Luis Enrique hakuwa na hofu ya Ramos kuzamisha penalti, baada ya kumpeleka ndiko siko kipa Rune Jarstein kufuatia mlinda mlango huyo kumwangusha Alvaro Morata eneo la hatari na kuzawadiwa tuta hilo.

"Sergio Ramos ni mchezaji wa kipekee katika historia ya soka duniani," kocha huyo wa Hispania aliiambia Teledeporte.

"Mchezaji mwenye sifa hiyo, najua atapiga vizuri."

Ramos alichukua jukumu hilo katika hatua za mwisho za mchezo na kuiwezesha Hispania kupata ushindi huo muhimu kwao.

"Sasa najisikia vizuri," Ramos aliongeza. "Nadhani usumbufu wa anguko utakuja baadaye.

## KWA UFUPI

**HUDSON-ODOI ATEGWA UNITED**

Manchester United imejiunga katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa England na Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 18. ***(Mail)***

**INTER BADO YAMTAKA RAKITIC**

Inter Milan bado inatumai kumsajili kiungo wa Barcelona, Mcroatia Ivan Rakitic, 31, na winga wa PSV Eindhoven, Mholanzi Steven Bergwijn, 21. ***(La Gazzetta dello Sport)***

**NKUNKU, SARR KUTUA ARSENAL**

Arsenal inatoa kipaumbele katika kumsaka beki mpya wa kushoto, winga mshambuliaji na mbadala wa Aaron Ramsey katika dirisha hili la majira ya joto. Kocha Unai Emery yupo tayari kuisaka saini ya kiungo wa Paris St-Germain, Mfaransa Christopher Nkunku, 21, na winga wa Rennes, Msenegal Ismaila Sarr, 21. ***(Football London)***

**KOULIBALY KUIGHARIMU UNITED**

Manchester United itapaswa kuvunja rekodi yao na kulipa pauni milioni 130 ili kumsajili beki wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly, 27. ***(Mail)***

**SKRINIAR AANDALIWA DAU CITY**

Manchester City inaandaa ofa ya pauni milioni 85 kwa beki wa Inter Milan, raia wa Slovakia, Milan Skriniar, 24. ***(CalcioMercato)***

**JOTA APIGIWA HESABU SPURS**

Tottenham inamfuatilia straika wa Wolves, Mreno Diogo Jota, 22, na kiungo wa Aston Villa, Muingereza Jack Grealish. ***(Express)***

**OVERMARS AICHOKONOA SPURS**

MKURUGENZI wa Soka wa Ajax, Marc Overmars, ameelezea kiu yake ya kuwarejesha mabeki wa Tottenham, Wabelgiji Jan Vertonghen, 31, na Toby Alderweireld, 30, katika klabu hiyo majira haya ya joto. ***(Fox Sports - via Metro)***

**VARANE AFICHUA KUONDOKA REAL**

BEKI wa Real Madrid, Mfaransa Raphael Varane, 25, amewaambia wachezaji wenzake anataka kuondoka hapo Bernabeu. ***(Marca - via Mirror)***

**EVERTON MAWINDONI KWA LEAO**

Everton imeulizia uwezekano wa kumpata straika wa Lille, Mreno Rafael Leao, 19, wakati huu ikitazama uwezekano wa kuongeza washambuliaji majira haya ya joto. ***(Mail)***

**CHELSEA, INTER KWA BARELLA**

RAIS wa Cagliari, Tommaso Giulini, amethibitisha kufanya mazungumzo na klabu kadhaa ikiwamo Chelsea na Inter Milan kuhusu kumuuza kiungo wao, Nicolo Barella, 21. ***(Corriere dello Sport)***

**SOUMARE LULU NEWCASTLE, SPURS**

Newcastle na Tottenham zitaingia vitani kuiwania saini ya kiungo wa Lille, Mfaransa Boubakary Soumare, 20. ***(Star)***

**NACHO, VALLEJO WANUKIA SOKONI**

MABEKI wa Hispania Nacho Fernandez, 29, na Jesus Vallejo, 22, wote kuna uwezekano wa kuwamo katika orodha ya wachezaji watakaouzwa na Real Madrid. ***(Mail)***



# MWAKINYO ALIVYOMCHAPA 'NDUGU' WA MESSI KWA KO

**Na Mwandishi Wetu, NAIROBI**

BONDIA Hassan Mwakinyo ameipeperusha vema bendera ya Tanzania baada ya juzi usiku kumshinda kwa Knockout (KO) mpinzani wake, Sergio Eduardo Gonzalez wa Argentina katika raundi ya tano kwenye pambano kali lililofanyika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Kenyatta (KICC) jijini Nairobi, Kenya.

Katika pambano hilo la uzito wa Super Welter ambalo lilikuwa la raundi nane, Mwakinyo alimsukumia makonde mazito bondia huyo ambaye ni 'ndugu' wa taifa moja na mchezaji nyota wa Barcelona, Lionel Messi, na kujikuta akisalimu amri raundi ya tano.

Mashabiki wengi waliamini kuwa huenda pambano hilo lingeamuliwa kwa pointi, lakini Mwakinyo alirudi kwa kasi ya ajabu katika raundi ya tano na kurusha makonde mfululizo ambayo yalimshinda Gonzalez.

Mwakinyo alionekana kutumia vema udhaifu wa Gonzalez upande wake wa kushoto ambao alikuwa akiulinda muda mwingi wa mchezo. Lakini makonde mawili ya nguvu kutoka kwa Mwakinyo yalitosha kumpeleka chini Gonzalez ambaye alishindwa kunyanyuka hali iliyomfanya mwamuzi kumalizika pambano hilo.

Aidha, taarifa kutoka jijini Tanga alikozaliwa Mwakinyo, zinaeleza kuwa mara baada ya pambano hilo kumalizika na bondia huyo kutangazwa mshindi, vifijo na nderemo zilipuka maeneo ya Makorora alipozaliwa mwanamasumbwi huyo ambaye ni balozi wa Kampuni ya SportPesa.

Hilo linakuwa pambano la tano mfululizo kwa Mwakinyo kushinda tangu Machi 10, mwaka jana, alipomshinda Ambokile Chusa kwa pointi jijini Dar es Salaam, kabla ya kwenda kumpiga Muingereza Sam Eggington Septemba 8, mjini Birmingham, Said Yazidu Oktoba 20, na Joseph Sinkala Oktoba 28, mwaka jana mjini Tanga, yote kwa KO.



Bondia Mtanzania Hassan Mwakinyo akimchapa konde bondia Sergio Eduardo Gonzalez wa Argentina katika pambano la uzito wa Super Welter lililofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Kenyatta (KICC) jijini Nairobi, Kenya juzi. Mwakinyo alishinda kwa KO. **PICHA: SPORTPESA**

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.YANGA | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.AZAM | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3.SIMBA | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4.LIPULI | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.KINONDONI MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6.MTIBWA SUGAR | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ PRISONS | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.COASTAL UNION | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.MBEYA CITY | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.ALLIANCE | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.MWADUI | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.KAGERA SUGAR | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT TANZANIA | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.MBAO | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15.STAND UTD | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.RUVU SHOOTING | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.SINGIDA UTD | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.NDANDA | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.BIASHARA UTD | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.AFRICAN LYON | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Kilichompa Kangwa mkataba Azam hiki

**Na Mwandishi Wetu**

MTENDAJI Mkuu wa klabu ya Azam FC, Abdulkarim Amin ' Popat', amesema benchi la ufundi la timu hiyo linafurahishwa na kazi ya beki wao, Bruce Kangwa na ndio sababu ya kumwongeza mkataba mpya.

**Kangwa, alisaini mkataba mpya wa miaka miwili kuitumikia klabu hiyo Ijumaa iliyopita na kumfanya sasa kuendelea kuwa hapo Chamazi hadi mwaka 2021.**

Akizungumza na Nipashe jana, Popat alisema Azam imekuwa na utaratibu wa kutathmini jitihada za mchezaji kupitia benchi la ufundi la klabu hiyo na hivyo Kangwa alistahili kupewa mkataba mpya.

"Kama Azam tumefurahi kuona Kangwa ameongeza mkataba wa kuendelea kuitumikia klabu yetu, kama klabu tumefurahi na tumeridhika na utendaji wake," alisema Popat.

Aidha, alisema kwa sasa wameelekeza nguvu kwenye michezo yao ya ligi hasa baada ya timu kuendelea kufanya vizuri.

Azam ilifanya mabadiliko ya benchi la ufundi kwa kumuondoa Kocha Mkuu Hans van der Pluijm na msaidizi wake, Juma Mwambusi na nafasi zao kukaimiwa na Abdul Mingange na Iddi Chechen.

# Cannavaro apuuza viporo Simba kulika

**Na Faustine Feliciane**

MENEJA wa vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga, Nadir Haroub ' Cannavaro' amesema, wanaojidanganya kuwa timu yao haiwezi kutwaa ubingwa kutokana na viporo vya watani zao, Simba 'kulika', wanajidanganya.

Cannavaro aliliambia Nipashe jana, kuwa ligi ya msimu huu ni ngumu na imekuwa na changamoto kubwa, lakini anaamini timu yake itaendelea kufanya vizuri.

Nahodha huyo wa zamani wa timu hiyo, alisema kuwa juhudi zinazofanyika kwao ni kuhakikisha wanafanya vema kwenye kila mchezo uliopo mbele yao.

**"Asikudanganye mtu, hakuna timu ambayo tayari ina uhakika wa ubingwa... kila timu ina pambana kushinda mechi zake, michezo bado ipo mingi na naamini sisi [Yanga] pia tupo kwenye mbio za ubingwa, " alisema Cannavaro.**

Alisema kwa sasa benchi la ufundi la timu hiyo linaelekeza nguvu kwenye mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Alliance ya Mwanza.

"Baada ya mchezo dhidi ya Alliance, tutaendelea na mikakati yetu ya michezo ya ligi, lakini kwa sasa nguvu tunaelekeza kwenye mchezo wetu wa FA," alisema Cannavaro.

Yanga itaumana na Alliance Machi 28, Alhamisi ijayo, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.



# Michezo

Jumatatu Machi 25, 2019

Nipashe




Ramos akunwa na falsafa za Enrique

HABARI UK 30



Mbwana Samatta (10), Simon Msuva (12) na Farid Musa, wakimpongeza Erasto Nyoni (4)baada ya kuifungia Stars bao la pili kwa mkwaju wa penalti wakati wakishinda 3-0 dhidi ya Uganda kwenye mechi ya kuwania kufuzu Afcon Juni nchini Misri. **PICHA: BIN ZUBEIRY**

# YAMETIMIA

## TANZANIA YATETEMA AFCON

●●●Bocco, Samatta, Msuva wafanya makubwa Taifa, historia mpya yaandikwa baada...

**Na Faustine Feliciane**

HATIMAYE baada ya miaka 39 Tanzania imefuzu kwa mara ya kwanza kushiriki fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon), kufuatia kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Uganda (Cranes) katika mechi yao ya mwisho ya hatua ya makundi, shukrani pia zikiiendea Cape Verde kutokana na kulazimisha sare tasa dhidi ya Lesotho kwenye mchezo mwingine wa Kundi L.

Kwa matokeo hayo, Tanzania inaungana na Uganda kushiriki fainali za Afcon nchini Misri Juni, mwaka huu, kutokana na kumaliza nafasi ya pili pointi tano nyuma ya vinara hao wenye alama 13.

Kwenye mchezo wa jana, Stars ilikuwa ikihitaji ushindi tu, huku ikiomba Lesotho kutoka sare au kufungwa na Cape Verde, dua ambazo zimepokelewa kufuatia timu hizo kutoka sare tasa.

Mshambuliaji Simon Msuva alikuwa wa kwanza kuwainua mashabiki walioujaza Uwanja wa Taifa kwa bao la kwanza dakika 21 kwa shuti la ndani ya boksi baada ya kupokea pasi safi ya John Bocco.

Baada ya bao hilo Stars iliendelea kuliandama lango la Uganda, huku wakishangiliwa na mashabiki wengi wakiongozwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, pamoja na viongozi wengine akiwamo Waziri wa Habari, Sanaa, Utamadumi na Michezo, Harrison Mwakyembe. Dakika ya 51, Erasto Nyoni aliipa Stars bao la pili kwa mkwaju wa penalti iliyotokana na kazi nzuri ya Mbwana Samatta aliyemchambua mlinzi mmoja wa Uganda na kuingia na mpira ndani ya boksi kisha kumnawisha beki mwingine na mwamuzi kuamuru litengwe tuta.

Baada ya bao hilo Stars ikitumia faida ya kuwa uwanja wake wa nyumbani, huku ikishangiliwa kwa nguvu zote, waliendelea kulisakama lango la Uganda ambapo Samatta, Bocco na Msuva waliendelea kuwa mwiba mchungu kwa mabeki wa wapinzani wao.

Beki Agrey Morris aliunganisha vizuri mpira wa krosi ya Bocco kutoka wingi ya kulia katika dakika ya 57 na kuiandikia Stars bao la tatu, hivyo kukata tiketi ya Misri. Kwa mara ya mwisho Tanzania kushiriki fainali hizo ilikuwa mwaka 1980 nchini Nigeria.

Kama Lesotho wangeshinda mchezo huo hata kama Stars wangeshinda kwa mabao 100 wasingefuzu fainali hizo.

Katika mchezo huo, kampeni ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda ya kuhamasisha Watanzania kujitokeza kwa wingi kushangilia Stars kwa asilimia 100 ilifanikiwa baada ya mashabiki wengi kujitokeza Uwanja wa Taifa na kuujaza.

# Yanga yamulika njia za Simba SC

**Na Faustine Feliciane**

KASI ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ni kama imewatisha mahasimu wao wakubwa, Yanga ambao sasa wanaomba 'Wekendu wa Msimbazi' hao wapoteze mchezo katika michezo yao saba ya viporo.

Yanga inaongoza ligi kwa kuwa na pointi 67 ikiwa ni pointi 13 zaidi ya Simba wanaoshika nafasi ya tatu, lakini ikiwa na michezo saba mkononi.

Kocha msaidizi wa timu hiyo, Noel Mwandila, aliliambia Nipashe jana, kuwa wao wamejikita kwenye michezo yao iliyo mbele, lakini pia wanaombea wapinzani wao, Azam na Simba wapoteze mechi zao.

**"Kila timu inacheza mechi zake, lakini kwa upinzani uliopo kila mmoja anamwombea mwenzake apoteze mchezo, kupoteza mchezo kwa wapinzani wetu na sisi tukifanya vizuri kuna wepesi kwetu," alisema Mwandila.**

Aidha, nahodha wa zamani wa timu hiyo, Kelvin Yondani, naye aliliambia Nipashe kuwa hawaangalii michezo ya timu nyingine zaidi ya timu yao.

Alisema kwa sasa ni kila timu ' inamwombea adui njaa', hivyo watajitahidi kuhakikisha wanashinda mechi zao, lakini pia wanawaombea wapinzani wao wapoteze mechi zao.

"Ligi ngumu, ushindani umeongezeka zaidi mzunguko huu wa pili... lakini tutapambana kuhakikisha tunafanya vizuri," alisema.

Baada ya mchezo wa jana wa timu ya Taifa ' Taifa Stars' dhidi ya Uganda, michezo ya Ligi Kuu na Kombe la FA itaendelea wiki

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >